

**KUCHUNGUZA TOFAUTI ZA KIMAANA KATI YA REJISTA YA MAKULI  
WA BANDARINI UNGUJA NA LUGHA SANIFU YA KISWAHILI**

**ABDALLA JUMA ABDALLA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA  
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A  
KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## **UTHIBITISHO**

Nathbitisha kwamba, aliyesaini hapo chini ameisoma tasnifu hii iitwayo **Tofauti ya Rejista ya Makuli Wa Bandarini na Lugha Sanifu Ya Kiswahili** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa Degree ya M.A Kiswahili ya ChuoKikuu Huria cha Tanzania.

.....  
**DKT: HANNA SIMPASA**

**(Msimamizi)**

**Tarehe.....**

**HAKI MILIKI**

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile kama vile kurekodi, kunakili kama ilivyo, kufuatanisha au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya Mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**TAMKO**

Mimi, **ABDALLA JUMA ABDALLA** nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa kazi kama hii inayozungumzia Makuli katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote

.....  
**ABADALLA JUMA ABDALLA**

**Tarehe .....**

## **TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa Mke wangu mpenzi, Zuwena Abdalla Ali hasa kwa kukubali kwake kunivumilia wakati wote wa masomo na pia watoto wangu Moh'd abdalla Juma, Far-hia Abdalla Juma pamoja na Rukia Abdalla Juma ili na wao iwape motisha wasome kwa bidii na kufikia kiwango cha juu zaidi ya mimi. Aidha nisimsahau Baba mzazi akiwa ni mzee aliyenipa moyo wakati wote wa mazingira magumu ya masomo

## SHUKURANI

Mwazo kabisa sina budi kumshukuru Mwenyeezi Mungu Muumba wa mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo kwa kunijaalia uhai, uzima, na kunipa uwezo wa kusoma hadi kufanya utafiti, kuandika na kuikamilisha kazi hii. Pili, napenda niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine tokea kuandaa hadi kukamilika kwa kazi hii. Hata hivyo, si rahisi kuwataja wote kwa majina, hata hivyo, ninapenda waelewe kwamba nimejali msaada wao na ninawashukuru sana. Hivyo, naomba wakubali na waungane na mimi kuwataja baadhi yao kwa niaba ya wote. Awali kabisa, shukrani nyingi na za pekee ziende kwa msimamizi wangu, Dkt. Simpasa, kwanza, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu, pili kukubali kwa moyo wake kuniongoza vizuri na kunirekebisha pale ambapo palihitaji marekebuisho. Dkt. Simpasa kwangu alikuwa ni mshauri, muelekezaji na mwalimu aliyenikosoa kwa busara na hekima kubwa kila ilipobidi kukosolewa na kuelekezwa. Ukweli ni kwamba kazi aliyofanya kwangu siwezi kuilipa kwa gharama yoyote ila namuomba Mwenyezi muungu ampe afya njema, ampe umri mrefu ili aweze kuwaongoza na kuwaelekeza wengine. Nahitimisha shukrani zangu kwake kwa kusema Mungu ambariki katika harakati zote za kimaisha akiwa ndani au nje ya Chuo Kikuu Huria.

Aidha, ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na wanataaluma wezangu wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za jamii, shukrani za ziada ziende kwa viongozi wa kituo cha Zanzibar kwa kunipokea na kunipatia kila aina ya msaada au ushauri niliouhitajia na kuifanya kazi yangu iwe rahisi na kukamilika kwa wakati. Kwa kuendelea, sitomsahau mwalimu wangu Bakari Kombo Bakari aliyekubali kupoteza siku na muda wake kutoka Pemba anakoishi kikazi na kuja Unguja kuniongoza, kunishauri na kunisaidia katika kukamilisha kazi hii ya utafiti

tokea maandalizi hadi kukamilika kwake sina cha kumlipa isipokuwa namuomba mwenyezi mungu ampe kila lenye heri katika maisha yake yote akiwa hapa duniani na akhera twendako.

Vile vile shukrani zangu maalum ziwaendee wazazi wangu wapendwa; Mama yangu marehemu, Miza Makame Hamdu na Baba yangu Mzazi Juma Abdalla Haji kwa kunilea kwa uangalifu mkubwa na kunisomesha hadi kufikia elimu ya juu katika uhai wao. Vile vile shukrani nyingi ziende kwa Marehemu Babu yangu Mzee Abdalla Juma Haji ambaye yeye alikuwa ndio mlezi wangu akiwa ni kiungo muhimu na ni kingowe katika kusaka elimu, alikuwa msitari wa mbele asubuhi na jioni na alihakikisha kila palipokuwa na shida ya kielimu aliikabili kwa mafanikio, Mwenyezi mungu amlaze mahala pema peponi Amina. Pia nawashukuru wadogo zangu wapendwa Sharifu Juma Abdalla , Kombo Juma Abdalla na Bi Semeni Juma Abdalla kwa mapenzi yao na huruma kubwa kwangu kwa michango yao mizuri. Nitafanya kosa kubwa tena la jinai nisipomtaja Mke wangu Bi. Zuwena Abdalla Ali , pamoja na watoto wangu wapendwa Moh'd Abdalla Juma, Far-hia Abdalla Juma , Rukia Abdalla Juma , Munawarat Abdalla Juma, Latifa Abdalla Juma pamoja na mjomba angu Miza Ramadhani kwa uvumilivu wao katika kuwabana wakati wa kulipia gharama za kimasomo, nawashukuru sana kwa uvumilivu wao. Mwisho napenda kuwashukuru wanafunzi wezangu wote waliosoma isimu ya lugha ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania katika mwaka wetu wa masomo 2017/18 kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kambi yetu ya masomo tukiongozwa na mwanafunzi mwezettu kiongozi Mwl. Shomar wa Skuli ya Vikokotoni Sekonrdari iliyopo Mjimi unguja.

## IKISIRI

Kazi hii inahusu kuchunguza tofauti ya rejista ya makuli wa bandarini Unguja na ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ambayo ni . Kubainisha sifa za rejista yamakuli wa bandarini katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Kuchunguza sababu kuibuka kwa tofauti kati ya rejista hii na Kiswahili sanifu, na kubainisha athari zinazotokana narejista ya makuli wa bandarini na watumiaji wengine wa lugha ya Kiswahili. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa, mbinu mbalimbali za utafiti zilihusika, ambazo ni hojaji, mahojiano pamoja na ushuhudiaji. Nadharia tatu zilitumika ambazo ni nadharia misimbo ya Bernstein, nadharia ya Giles ya maafikiano ambapo tumeangalia mazungumzo ya makuli wao wenyewe na wateja wao pamoja na nadharia ya vitendo usemi iliyoasisiwa na kuelezwa na mtaalamu Austin na Searle kwa kujikita katika mazungumzo baina ya makuli na wateja wao. Utafiti uligundua kwamba mazungumzo baina ya makuli na matajiri wao yamedhihirisha matumizi ya misimbo pana na misimbo finyu. Pia tumegundua kwamba kuna maafikiano baina ya makuli kama kikundi cha jamii kutokana na matumizi ya lugha yao. Mazungumzo baina ya makuli na matajiri wao yamedhihirisha kutokea kwa vitendo usemi ambavyo vinadhihirisha athari ya rejista ya makuli. Vile Vile utafiti umebaini kwamba usemi wa makuli wa bandarini umedhihirisha vitendo usemi ambavyo huwa na sifa ya kutambulika kutokana na kinachosemwa. Ili kutaka kujua athari ya kitendo fulani, sharti kuangalia kinachosemwa, kinasemwa wapi, na nani na kwa nani. Mtafiti amependekeza mambo kadha na kwa tafiti zijazo zitanue wigo na kufanyia kazi maeneo mengine Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kufanya utafiti kwa kuangalia tofauti baina ya rejista ya makuli wa bandarini Unguja na rejista ya makuli wa bandari ya Dar salaama na kufanya utafiti baina ya makuli wanaobeba mizigo na makuli wanaobeba samaki bandarini feri Dar-salaam.



## YALIYOMO

|  |          |
|--|----------|
| UTHIBITISHO .....                        | i        |
| HAKI MILIKI.....                         | ii       |
| TAMKO.....                               | iii      |
| TABARUKU .....                           | iv       |
| SHUKURANI.....                           | v        |
| IKISIRI .....                            | vii      |
| YALIYOMO.....                            | viii     |
| ORODHA YA MAJEDWALI.....                 | xii      |
| ORODHA YA PICHA.....                     | xiii     |
| ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA .....  | xiv      |
| <br>                                     |          |
| <b>SURA YA KWANZA .....</b>              | <b>1</b> |
| <b>UTANGULIZI NA USULI WA MADA .....</b> | <b>1</b> |
| 1.1 Utangulizi.....                      | 1        |
| 1.2 Usuli wa Mada .....                  | 2        |
| 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti.....      | 7        |
| 1.4 Malengo ya Utafiti .....             | 8        |
| 1.4.1 Lengo kuu .....                    | 8        |
| 1.4.2 Malengo Mahasusi .....             | 8        |
| 1.5 Maswali ya Utafiti .....             | 8        |
| 1.6 Umuhimu wa Utafiti .....             | 9        |
| 1.7 Mipaka ya Utafiti .....              | 10       |
| 1.8 Changamoto za Utafiti .....          | 10       |

|   |   |           |
|---|---|-----------|
| 1.9   | Mpangilio wa Utafiti.....                               | 11        |
| <b>SURA YA PILI.....</b>                                      |   | <b>12</b> |
| <b>MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .....</b> |   | <b>12</b> |
| 2.1   | Utangulizi.....   | 12        |
| 2.2   | Ufafanuzi wa Istilahi.....                              | 12        |
| 2.2.1   | Lugha Kama muhimili wa Mawasiliano.....                 | 13        |
| 2.2.2   | Dhana ya Rejista .....                                  | 13        |
| 2.3   | Mifano ya Rejista.....                                  | 17        |
| 2.4   | Rejista ya Makuli wa Bandarini Unguja.....              | 22        |
| 2.5   | Kazi nyingine Zilizosaidia Utafiti Huu.....             | 24        |
| 2.6   | Mkabala wa Kinadharia .....                             | 32        |
| 2.6.1   | Dhana ya Nadharia.....                                  | 32        |
| 2.6.2   | Nadharia ya Isimujamii ya Misimbo (Bernstein 1964)..... | 33        |
| 2.6.3   | Nadharia ya Maafikiano ya Giles (1979).....             | 35        |
| 2.6.4   | Nadharia ya Vitendo Usemi (Austin na Searle 1975).....  | 38        |
| 2.7   | Hitimisho.....  | 41        |
| <b>SURA YA TATU.....</b>                                      |   | <b>42</b> |
| <b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>                                  |   | <b>42</b> |
| 3.1   | Utangulizi.....   | 42        |
| 3.2   | Aina ya Utafiti.....                                    | 42        |
| 3.3   | Eneo la Utafiti .....                                   | 43        |
| 3.4   | Walengwa wa Utafiti .....                               | 44        |
| 3.5   | Sampuli na Usampulishaji .....                          | 45        |

|  |   |           |
|--|---|-----------|
| 3.5.1  | Sampuli .....   | 45        |
| 3.5.2  | Sampuli Kielelezo .....   | 46        |
| 3.5.3  | Usampulishaji .....   | 48        |
| 3.5.4  | Usampulishaji Welekeo .....   | 49        |
| 3.6  | Njia na mbinu mbali mbali zilizotumika katika kukusanya data .....            | 50        |
| 3.6.1  | Kompyuta.....   | 51        |
| 3.6.2  | Shajara.....  | 51        |
| 3.6.3  | Kamera .....  | 51        |
| 3.6.4  | Kinasa sauti .....  | 52        |
| 3.7  | Mbinu ya Hojaji .....   | 52        |
| 3.7.1  | Mbinu ya ushuhudiaji .....  | 53        |
| 3.7.2  | Mbinu ya mahojiano /usaili .....  | 54        |
| 3.8  | Uthabiti wa njia za kukusanya data.....                                       | 55        |
| 3.9  | Hitimisho.....  | 56        |
| <b>SURA YA NNE .....</b>                       |   | <b>57</b> |
| <b>UCHAKATAJI NA UCHANGANUZI WA DATA .....</b> |   | <b>57</b> |
| 4.1  | Utangulizi.....   | 57        |
| 4.2  | Tofauti ya kimaana kati ya rejista ya makuli na lugha ya kiswahili sanifu ... | 59        |
| 4.3  | Sababu za Kuibuka Rejista ya Makuli Bandarini Unguja .....                    | 60        |
| 4.4  | Athiri ya Rejista ya Makuli kwa Wanajamii Wengine .....                       | 62        |
| 4.4.1  | Mahusiano ya Lugha na kundi Lengwa la Jamii ya Makuli .....                   | 63        |
| 4.5  | Hitimisho.....  | 67        |

|   |           |
|---|-----------|
| <b>SURA YA TANO .....</b>                         | <b>68</b> |
| <b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>  | <b>68</b> |
| 5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti.....          | 68        |
| 5.2 Mapendekezo kwa wasomi na watafiti wajao..... | 69        |
| 5.3 Hitimisho.....                                | 70        |
| <b>MAREJELEO .....</b>                            | <b>71</b> |
| <b>VIAMBATANISHO .....</b>                        | <b>75</b> |

**ORODHA YA MAJEDWALI**

|            |   |    |
|------------|---|----|
| Jedwali 1  | Inaonyesha mgawanyo wa idadi ya makuli hamsini na nne waliofanyiwa utafiti. kama ni Sampuli ya Watafitiwa wakiwa ni miongoni mwa kundi lengwa. .... | 48 |
| Jedwali 2  | Walengwa kulingana na Umri wao. ....  | 48 |
| Jedwali 3. | Inaonyesha idadi ya makuli na kiwango cha Majibu kilichotolewa baada ya uchanganuzi wa taarifa zilizokusanywa. ....                                 | 58 |

### ORODHA YA PICHA

|             |   |    |
|-------------|---|----|
| Picha 1     | Makuli wakiwa katika harakati zao za kazi hapo bandarini huku wakitumia rejista zao mfano nipe nyuma, au ‘semile huko, semile huko’ .....   | 23 |
| Picha 2:    | Makuli wakipakuwa mzigo kutoka jahazini katika gati (bandari) ya majahazi iliopo mjini Unguja wakitumia ngazi ya mbao isiyo rasmin.....   | 24 |
| Picha no.3  | Picha hii inaonyesha Eneo la utafiti ( bandarini ) Unguja ambako rejista ya makuli hutumika katika kufanikisha kazi ya ukuli hapo bandarini. ....   | 44 |
| Picha no: 4 | Inaonyesha baadhi ya walengwa wa utafiti ambao ni makuli wakiwa katika harakati za kubeba mizigo kutoka katika boti la abiria linaotokea Dar- es- salama mara lilipowasili katika bandari ya malindi iliopo mjini unguja..... | 45 |

**ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

BAKIZA Balaza la Kiswahili Zanzibar

NK Nakadhalika

TUKI Taasisi ya Kiswahili

TYA Tayari ameshatajwa

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI NA USULI WA MADA**

#### **1.1 Utangulizi**

Lugha ni nyezo moja kuu ya mawasiliano kati ya mtu na mtu, jamii na jamii au hata Taifa na Taifa. Lugha inatumiwa na watu wa aina mbali mbali katika shughuli zao za kila siku mfano kupashana habari, biashara, kilimo michezo, kujifunzia na pia hutumika katika vyombo vikuu vya dola (Serikali, Bunge, mahakama) pamoja na shughuli nyingine za wanajamii mfano harakati za usafiri wa majini, nchi kavu pamoja na usafiri wa angani.

Matumizi ya lugha Kama nyezo muhimu ya mawasiliano yanaweza kuleta mabadiliko yenye athari chanya au hasi katika jamii kutegemea na watumiaji wa lugha. Kwa upande wa athari chanya, lugha yaweza kutumiwa kuwaunganisha watu na kuondosha chuki, hasira kejeli, dharau au uhasama miongoni mwa wanajamii lugha. Hata hivyo, lugha yaweza kuwa na athari hasi hasa ikiwa itatumiwa kuleta uhasama au kusababisha utengano baina ya mtu na mtu, jamii na jamii au hata makundi ya kijamii. Lugha huweza kuathiri mtazamo na tabia ya mtu. Yote hutegemea namna lugha inavyotumiwa ili kuleta athari iliyokusudiwa. Watu hutambua kikundi chao cha kijamii kutegemeana na misimbo au aina ya lugha wanayotumia. Matumizi ya lugha ndio huwafungamanisha watu wa kikundi fulani pamoja na kuwatambulisha.

Utafiti huu rejista ya wafanyakazi wa bandarini hasa makuli wa bandarini Unguja kwa kutumia mtazamo wa Isimujamii. Lugha ya makuli wa bandari ya Unguja ilichunguzwa katika muktadha mahsus; yaani mazingira ya kazi ambayo



yalimuwezesha mtafiti kuchunguza matumizi ya lugha na mtindo wao wa kuzungumza na hali zinazosababisha uzungumzaji wa namna fulani na athari zunazotokana na rejista hiyo kwa wasafiri na wageni wengine wanaotumia bandari ya Unguja.

## **1.2 Usuli wa Mada**

Makundi mbalimbali ya kijamii huwa na namna yao ya kipekee ya kuwasiliana, wafanyakazi wa bandarini kama kikundi cha kijamii wana upekee wao wa kuwasiliana. Lugha iliweza kutumiwa kutambulisha kikundi hiki cha wafanyakazi wa bandarini. Makuli wa bandarini wana jukumu la kubeba na kupakuwa mizigo bandarini. Lugha ni Chombo muhimu cha kuwawezesha makuli wa bandarini kuyafikia malengo yao na kuhakikisha kazi inafanywa vizuri na kwa ufanisi wa hali ya juu kupitia matumizi ya lugha (rejista). Kikundi hiki cha kijamii kinaweza kutofautishwa na vikundi vingine katika mkabala wa rejista yao. Kama asemavyo Gumperz (1972: 219), kikundi cha watu ambao wana sifa ya kuwa na mawasiliano yanayoendelea kila mara miongoni mwao kwa kutumia kundi lile lile la ishara za sauti, kikundi hicho cha watu kinatofautishwa na vikundi vingine kwa tofauti ya matumizi ya lugha. Kutokana na maelezo haya ya Gumperz, kikundi fulani huwa na lugha yake ya kipekee kutokana na mazoea ya muda mrefu, kuishi pamoja na kushirikiana. Kwa sababu hii kikundi huwa na makubaliano yasiyo rasmi lakini ambayo yanawatambulisha. Hii inaonyesha kuwa lugha ya kwanza katika kikundi fulani inaweza kubainishwa na kutumiwa kukitambua kikundi hicho. Makuli wa bandarini kufanya kazi ya kubeba mizigo wakati wote na kutumia lugha ya kikundi chao bila ya kuzingatia lugha zao za asili. Pamoja na kuwa utafiti wa rejista ya

wafanyakazi wa bandarini ni muhimu katika jamii ya Watanzania lakini bado utafiti wa kina haujaweza kufanywa kwa kuichanganua na kuibainisha rejista hiyo katika utekelezaji wa majukumu ya walengwa hao. Ndio maana mtafiti aliamua kuchagua na kuishughulikia mada hii. Makuli wa bandarini hufanya kazi ya kubeba mizigo wakati wote na kutumia lugha ya kikundi chao bila ya kuzingatia lugha zao za asili. Hoja ya lugha kuwa utambulisho inaungwa mkono na Wamitila (2003) ambaye anadai kuwa, lugha ndio nyezo kuu ya mawasiliano. Dhamira au malengo makuu ya mawasiliano yoyote yale yanayotumia lugha, hayawezi kuwasilishwa na kuwafikia walengwa bila ya kuwepo taaluma sahihi ya isimu jamii. Jamii ndio chimbuko la njia tofauti za mawadiliano ikiwemo lugha Kila jamii mawasiliano ni kitu muhimu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Kikundi chochote kile huwa na namna yao ya kipekee ya kutumia lugha na kutofautiana na kikundi kingine. Maelezo haya yanaungwa mkono na mwanaisimu Habwe na wengine (2010:71) kwa kusema, ili kukidhi haja ya mawasiliano, makundi ya kijamii huibua mitindo na istilahi zao zinazowawezesha kurejelea shughuli za kundi husika. Hii inaashiria kuwa kila kikundi katika nyanja mbalimbali huwa na mtindo wake wa kutumia lugha kwa namna ambayo itawawezesha kufikia malengo ya kazi zao. Wafanyakazi wa bandarini kama kikundi cha kijamii pia wana rejista zao ambazo huwawezesha kutekeleza majukumu yao na huwa ndio utambulisho wao. Kwa sababu hii, mtafiti alichunguza rejista ya wafanyakazi wa bandarini ili kubaini lugha ya kikundi hicho na tofauti iliopo na lugha sanifu ya Kiswahili. Kikundii hiki cha wafanyakazi wa bandarini Unguja kiliweza kutambuliwa kutokana na rejista yao kwa kuchunguza tofauti zilizopona lugha sanifu ya Kiswahili. Kama asemavyo Bernstein (1964) tofauti za kiisimu za matumizi ya lugha ya kikundi fulani hutokea katika mazingira

halisi ya kijamii na vyeo vya makundi mbalimbali huweza kubainishwa nausemi wao. Fishman (1972) anasema, jamii ni ya muhimu na kwa hivyo jamii ya makuli wa bandarini unguja ilituwezesha kuchunguza rejista yao hasa wanapokuwa katika harakati za kupakuwa mizigo na kusafirisha abiria kwa kuwa hayo ndio mazingira yanayowatambulisha na ndio muktadha wao halisi.

Fishman (1968:139) akimnukuu Halliday (1978) anasema, uchunguzi wa muktadha wa mazungumzo hutuelekeza katika uchanganuzi wa hali na matumizi ya lugha. Kutokana na ukweli huu, tumeweza kuchunguza na kuchanganua rejista ya wafanyakazi wa bandarini hasa makuli. Katika kufanikisha uchunguzi huo tumezama zaidi katika eneo la bandari ya Malindi iliyopo mjini Unguja ikiwa ni eneo la utafiti huu. Kama anavyowa msisitizo, Pride (1971:25) Kwa kusema, mawanda au eneo la matumizi ya lugha ni mahali ambapo matumizi ya aina fulani ya lugha hutumiwa na kikundi mahsusi na hii husaidia katika utambulisho wa kikundi hicho cha kijamii. Hii inaashiria kuwa kikundi fulani cha watu huweza kuainishwa kijamii na kiisimu. Katika kuchunguza rejista ya wafanyakazi wa bandarini tumekichunguza kama kikundi cha kiisimu jamii. Naye Hirst (1986) anasema, kadri ya matumizi ya lugha yanavyokua, husababishwa na watu wenyewe binafsi au pia wao wanasimama kama wanajamii. Hii ina maana kwamba, lugha wanayotumia katika mazungumzo huchangia katika kujitambua na kudhihirisha kama kikundi husika. Wafanyakazi wa bandarini nao ni jamii, hivyo lugha wanayoitumia huwatambulisha kama kikundi cha wafanyakazi hao wakiwemo makuli na wafanyakazi wengine wa bandarini Unguja. Kwa kuzingatia maelezo ya wataalamu hawa, ni wazi kwamba wafanyakazi wa bandarini wana msimbo fulani wa mawasiliano ambao wanauelewa wao wenyewe tu.

Kwa mfano makuli wanaposema “*nipe nyuma* “(rejista), huwa na maana ya “**anahitaji njia ya kupita akiwa amebeba mzigo** “ maana ambayo ni tofauti na ile maana inayojulikana katika lugha sanifu ya Kiswahili ambapo inamaanisha muhusika aliyeomba nyuma huwa anahitaji sehemu ya makalio au sehemu nyingine nyuma ya mwili wa binadamu. Msimbo wao ni finyu na hivyo waliweza kupata nafasi ya kujitenga na makundi mengine kama anavyosema mtaalamu Mukhwana (2011: 45). kwamba, katika msimbo finyu, wazungumzaji huweza kutumia ujuzi na maarifa yao katika mawasiliano kama ni mtindo wao wa mawasiliano. Wafanyakazi wa bandarini hutumia msimbo huo kama njia ya kuonyesha umoja na mshikamano katika kundi hasa wakati wa kazi zao za uhebaji na upakuzi wa `mizigo. Kwa sababu msimbo wanautumia ni kwa ajili ya kundi maalumun na katika mazingira maalumu hiyo tunaita Rejista yao, katika eneo lao la kazi kama zilivyo rejista za hotelini, hospitalini msibani, kanisani, msikitini na maeneo mengine ambako makundi maalumu hutambulishwa na lugha wanayotumia. Neno Rejista limeweza kufasiliwa na wataalamu mbali mbali kwa mfano:

Oxford Dictionary wanasema, rejista ni mtindo wa lugha inayotumika mahali penye shughuli fulani na ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida. TUKI (1990), rejista ni matumizi ya lugha kulingana na muktadha maalumu. Hii ina maana kuwa muktadha tofauti husababisha aina mbali mbali za lugha ambazo ndiyo huitwa Rejista. Baadhi ya vipengele vya muktadha ni mada, eneo la matumizi ya lugha, mahusiano baina ya wahusika, umri, jinsia, wakati na mambo mengine. Wataalamu hao wanatoa mfano wa Rejista ya kisheria, biashara, sayansi, dini na nyinginezo. Halliday (1978 ), rejista inahusu sura mbali mbali za lugha kulingana na tofauti ya matumizi yanayohusisha

matumizi mahsusi ya jamii kama vile matangazo, ibada, mambo ya kisiasa hata majadiliano ya kitaalamu na dhamira nyenginezo, Mwasiko (1991 ) anasema, rejista ni matumizi ya lugha kulingana na kufuatana na utendaji kazi wa lugha. Moody (1968), naye anasema kuwarejista ni namna ya kuwasilisha mawazo kwa njia tofauti kulingana na muktadha kama vile ambavyo mtu anaweza kuwa na nguo za kazi, kanisani/msikitini, msibani/sherehe naza shughuli nyingine. Mgullu (1999), anasema, tunatumia maneno haya mawili yaani: “sajili na rejista” Kama visawe. Kwa ujumla lugha zote ulimwenguni huwa na rejista zake ingawa lugha zilizoendelea huwa na rejista nyingi zaidi kuliko zile ambazo bado zinaendelea. Naye Mathoko (2007) anasema, sajili ya lugha ni mtindo wa lugha ambao hutegemea muktadha wa kijamii, kisayansi, dini, ualimu, sheria na nyenginezo. Anazidi kusesitiza kwamba, sajili inaweza kuelezwa Kama matumizi ya lugha katika viwango maalumu;kwa mfano, maongezi ya kawaida, sheria, biashara, kandanda, ukulima na teknolojia. Matumizi yanayohusika hutawaliwa na masharti, kama cheo, umri, muktadha, mahusiano ya kijamii, hali ya mtu na utamaduni. Kisumba (2011), anazungumzia kuhusu sajili ya sokoni na jinsi zinavyochangia katika kukuza misamiati ya Kiswahili. Kisumba anaeleza kwamba rejista ni taaluma muhimu sana ambapo ikitumiwa vyema inaweza kuongeza idadi kubwa ya msamiati wa lugha hata hivyo wasiokuwa na uelewa wa taaluma hiyo hupata mkanganyiko mkubwa katika matumizi ya rejista hizo. Kwa upande wa Wamitila (2003) katika matumizi ya lugha anasema, Lugha ndio nyezo kuu ya mawasiliano. Dhamira na maudhui katika mawasiliano yoyote yale katika lugha hayawezi kuwasilishwa na kuwafikia wasomaji bila ya kuwepo taaluma sahihi yan isimu jamii.

Kwa ujumla tunaweza kufasili rejesta kuwa ni mtindo wa lugha kutegemeana na kazi fulani, muktadha wa matumizi, lengo na uhusiano wa wanaowasiliana. Katika muktadha rasmi rejesta hurejelea upande mmoja kama vile, msamiati wa kiufundi, adabu maalum na matumizi ya lugha fasaha, mfano katika elimu, mahakamani na kadhalika. Rejista siku zote husimama kama ni utambulisho wa kundi fulani katika jamii na hutumika kuonyesha mahusiano ya kundi hilo kupitia mawasiliano yanayotolewa katika muktadha maalumu mfano: bandarini, Hospitalini, hotelini shuleni na maeneo mengine. Vile vile rejista ina nafasi kubwa sana katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Hii ni kutokana na kwamba, madhumuni makuu ya mawasiliano katika upakuaji na ubebaji wa mizigo unaofanywa na makuli wa bandarini na wafanyakazi wengine wa bandarini ni kurahisisha kazi yaani wahusika wafanye kazi kwa ari, kwa haraka bila ya kuonyesha kuchoka au kutegea na hatimaye kujiongezea kipato chao.

### **1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Watafiti mbali mbali wamejaribu kufanya tafiti zinazohusu matumizi ya rejesta za aina mbali mbali, mfano, rejista za shuleni, hotelini, hospitalini, polisi, vyuoni na maeneo mengine. Hata hivyo eneo la bandarini ambako nako liko kundi maalum la wanajamii (Kama makuli) ambao kazi zao ni za ubebaji na upakuaji wa mizigo wana rejista yao ambayo huwatambulisha kama kundi moja ambalo linaonekana kutopewa umuhimu katika tafiti zilizofanyika. Vile vile kutokana na ukweli kwamba rejista huweza kuwa na mchango wa kukuza msamiati wa lugha kama Kiswahili mtafiti wa utafiti huu aliona uwazi ambao haujafanyiwa utafiti Kwa kina na kuamua kufanya uchunguzi juu ya tofauti ya rejista inayozungumzwa na wafanyakazi wa bandari ya

Malindi iliopo mjini Unguja na lugha ya Kiswahili sanifu ili kuweza kubaini rejista inaotumika, sababu za kutumia rejista hiyo na vile vile kubaini athari ya rejista hiyo kwa watu wengine wanaotumia Kiswahili sanifu.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

##### **1.4.1 Lengo kuu**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza tofauti ya kimaana kati ya rejista inayozungumzwa bandarini Unguja na lugha ya Kiswahili sanifu.”

##### **1.4.2 Malengo Mahasusi**

Malengo ya utafiti huu yalijikita katika maeneo matatu makuu nayo ni;-

- a) Kubainisha tofauti ya kimaana kati ya rejista ya makuli wa bandarini unguja na lugha ya Kiswahili sanifu.
- b) Kubainiaha sababu iliyosababisha kuibuka kwa rejista hiyo katika eneo la bandarini Unguja.
- c) Kubainisha athari zinazotokana na rejista hiyo kwa watumiaji wengine.

#### **1.5 Maswali ya Utafiti**

Katika utafiti huu maswali ya utafiti yalikuwa Kama ifuatavyo:

- a.) Je? Kuna tofauti yoyote ya kimaana kati ya rejista ya makuli wa bandari ya unguja na lugha ya kiwsahili sanifu.
- b.) Ni sababu zipi zilizochangia kutokea kwa rejista hiyo?
- c.) Rejista ya makuli ina athsri gani kwa watumiaji wengine?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii tena kwa watu wa aina na rika tofauti hasa kwa kule kupata maana halisi na sahihi iliyokusudiwa na kuondoa dhana potofu inayoweza kujenga chuki na kusababisha ugomvi kwa wanajamii. Mfano mtu wa kawaida ambaye yuko mbali na mazingira ya watu wa kundi hili la makuli wa bandarini akisikia **“nipe nyuma”** ni kununua ugomvi usio na sababu, kwani muhusika huyo atajenga dhana kwamba kijana huyu anahitaji makalio yangu au mgongo wangu kitendo ambacho sio sahihi, hivyo utafiti huu utaondoa tatizo hilo Pia utafiti huu utakuwa ni kumbukumbu katika maktaba ambapo wasomi wajao watasoma na kuelewa uwepo wa aina hii ya rejista ya makuli wa bandarini na vile vile kubaini tofauti ya kimaana kati ya rejista inayotumiwa na kundi hilo maalumu katika mazingira ya bandarini na lugha ya Kiswahili Sanifu. Aidha wageni na watafiti mbali mbali watafika maktaba na kupata taarifa muhimu kuhusu rejesta hii na kuweza kufanya ulinganishi na rejista za makundi mengine ya kijamii kwa faida ya vizazi husika na vijavyo ndani na nje ya nchi.

Vile vile utafiti huu utasaidia taifa katika mambo ya kisera kwani kila taifa hupata maendeleo kutokana na tafiti mbali mbali zilizofanywa na wasomi na wataalamu mbali mbali mfano katika maendeleo ya elimu kwa ngazi mbali mbali. Sera ya elimu inahitajika katika kuandaa mtaala wa kufundisha njanja na mikondo mbali mbali ya kitaaluma. Kwa kumalizia utafiti huu utakuwa ni kichocheo kikubwa katika kukamilisha kazi za watafiti wengine watakaofanya utafiti unaolingana na utafiti huu.



### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Katika utafiti huu mtafiti alishughulikia eneo maalumu ambalo ni mazingira ya bandarini unguja ambapo meli na vyombo mbali mbali hutia nanga na vile vile makuli wanafanya kazi ya hupakia na kuteremsha mizigo na abiria. Katika eneo hilo, mtafiti alichunguza tofauti ya kimaana kati ya rejista inaozungumzwa na makuli na lugha ya Kiswahili Sanifu. Aidha mtafiti hakuhusika na miundo au mipangilio ya sentensi au sehemu nyingine yoyote ya isimu ya lugha. Katika utafiti huu, tulichunguza namna kipengele cha lugha kinavyotumika katika kuwatambulisha makuli wakiwa katika sehemu yao ya kazi. Makuli wa bandarini ni kikundi maalum cha kijamii. Hata hivyo, hatukuzama katika lugha yao ya asili ambayo wanaitumia mara tu watokapo bandarini. Kwa hivyo, katika utafiti wetu, tulichanganua data iliyohusu mambo ya kijumla yanayohusu rejista ya makuli.

### **1.8 Changamoto za Utafiti**

Haikuwa rahisi kukamilisha ukukusanyaji wa data kutoka kwa makuli katika eneo la bandari ya Malindi iliyopo mjini Unguja. Ilimlazimu mtafiti kutafuta mtu atakayemuongoza ambaye ni afisa wa bandari katika sehemu hiyo. Makuli wa bandarini walipigwa na butwaa kuwepo kwa mtafiti hapo bandarini muda wote. Eneo la bandarini kama linavyoeleweka huwa na harakati nyingi za kazi za uchukuzi na hivyo kuwapata makuli inakuwa sio rahisi sana na muda wao wa mazungumzo huwa mfupi mno. Nililazimika kurekodi mazungumzo yao kwa wakati tunaowapata na wakati mwingine tulirekodi mazungumzo ya dakika chache sana. Hatukuwa na uwezo wa kuwazuia au kuwafanya waendeleo na mazungumzo kwa kuwa kazi za uchukuzi zlikuwa nyingi na matajiri wao walihimiza kazi zao zifanywe haraka.

## 1.9 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu una tano. Sura ya kwanza inazungumzia usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu na malengo mahasusi ya utafiti, umuhimu, mipaka, pamoja na vikwazo vya utafiti. Sura ya pili imezungumzia kazi tangulizi mbali mbali na ambapo mtafiti ameweza kupitia kwa kusoma makala na kazi mbali mbali za watafiti waliotangulia. Katika sehemu hii mtafiti ameangalia nyaraka na kazi mbali mbali zilizofanywa na watafiti waliotangulia hasa zile zinazohusiana au zinazofanana na mada ya mtafiti yaani **”rejista”/sajili”**. Katika utafiti huu, sura ya tatu ambayo mtafiti anazungumzia mbinu za utafiti na kueleza aina ya utafiti, sampuli na usamplishaji, pamoja na kueleza uthibiti wa njia za utafiti na kukusanyia data. Sura ya nne imewasilisha na kuchambua data za utafiti; ilhali sura ya tano imetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii imezungumzia mapitio ya machapisho yaliyoandikwa ikiwa ni sehemu ya kazi tangulizi mbalimbali zilizopata kuzungumzia mada inayofanana au kukaribiana na mada iliyofanyiwa utafiti yaani “rejista” pamoja na kutaja nadharia zitakazoongoza utafiti huu. Kazi tangulizi zilizopitiwa na mtafiti zimeelezea aina mbali mbali za rejista na namna zilivyojitokeza katika makundi mbali mbali duniani. Mtafiti katika sehemu hii ameangalia rejista mbali mbali na namna zilivyofanyiwa uchunguzi na kuona matokeo ya uchunguzi huo ambao umetoa mwanga mzuri wa kukamilisha utafiti huu. Aidha lengo kuu la mapitio ya kazi tangulizi ni kupata kuona ni kwa kiasi gani wanaisimu wamezungumzia matumizi ya rejista ndani ya lugha moja au eneo moja ambako kuna kundi fulani lenye kutumia rejista kama utambulisho wao. Majibu ya tafiti hizo yamemsaidia sana mtafiti kubaini kuwa yapo maeneo mengi ambayo kuna makundi ya watu maalumu kulingana na kazi au shughuli wanazozifanya. Wanajamii huona aina fulani na ya kipekee ya mawasiliano ambayo pia huwa ndio utambulisho wao na ni tofauti na makundi mengine hata kama wanatumia lugha ya aina moja lakini bado hayajafanyiwa uchunguzi wa kina. Hivyo, kutokana na mapitio hayo mtafiti ameona kuna umuhimu wa kufanya utafiti zaidi kuhusu matumizi ya rejista katika mazingira ya bandarini ili kuongeza maarifa mapya katika kipengele hiki cha rejista katika uwanja wa lugha ya Kiswahili.

#### **2.2 Ufafanuzi wa Istilahi**

Katika sehemu hii tumefafanua dhana kadhaa kama ifuatavyo:

### **2.2.1 Lugha Kama muhimili wa Mawasiliano**

Wataalamu mbali mbali wametoa tafsiri ya neno lugha kwa kuzingatia mitazamo na vigezo mbalimbali. Baadhi ya wataalamu waliofafanua dhana ya lugha mfano, Lado (1964), Nkwera (1989), kamusi ya Kiswahili Sanifu (1990:35) na wengineo. Wataalamu hawa wote kwa ujumla katika fasili zao yanafanana kwa kiasi kikubwa na wanakubaliana kwamba lugha ni chombo cha mawasiliano ya wanaadamu ambacho hukitumia katika kupashana habari miongoni mwao wakiwa na sifa ya kuwa na utamaduni wa aina moja na pia wamezidi kutoa ufafanuzi kwamba ili mawasiliano yakamilike lazima kuzingatia mambo muhimu na ya msingi kama sauti za nasibu, maana, mawasiliano, binaadamu, na utamaduni wa aina moja.

### **2.2.2 Dhana ya Rejista**

Neno rejista limeweza kufafanuliwa na wataalamu wengi. Kwa kuanzia na Iribemwangi na Mukhwana (2011:19) wanaema, rejista katika taaluma ya isimujamii humaanisha mikondo ya kimawasilian itumiwayo katika hali na muktadha fulani fulani kwa madhumuni maalum. Wanaendelea kutaja mambo yanayoathiri rejista aliyozungumzia mwanaisimu Halliday, kwamba ni Utaratibu wa mahusiano ya maisha. Huu ni uhusiano baina ya mzungumzaji na mzungumziwa, Uwanja unaozungumziwa mada zinazozungumziwa na mahala ni muhimu katika kufafanua rejista husika na Mtindo au namna ya kuwasiliana. hawa wanasema kuwa rejista hujitokeza wazi katika mazingira fulani mahsusi. Hii ina maana kuwa rejista hutofautiana kutegemea na muktadha na kikundi fulani cha kijamii. Mtu binafsi anaweza kuwa na rejista mbalimbali kutegemea na hali yake, kazi, malengo na hata cheo chake. Mtu huyo huyo anapokwenda harusini Kwa mfano, atatumia rejista

tofauti na anapokwenda hospitalini mazungumzo huwa ni ya mtindo tofauti ambao kutegemea vitu kama, mada, muktadha, uhusiano na pia lengo la mzungumzaji. Makuli wa bandarini Unguja wana madhumuni sawa na hiyo wanapokuwa bandarini wanatumia lugha kwa njia sawa. Hudson (1993) anasema kuwa rejista ni matumizi ya lugha kutegemea na muktadha. Hii inaonyesha kuwa, muktadha wa mazungumzo huathiri lugha inayotumiwa. Maoni haya yanaoana na ya Trudgill (2000: 81) anasema lugha hutofautiana kutegemea tabia za wazungumzaji kama vile; tabaka, jamiilugha, jinsia lakini pia kutegemea na muktadha ambapo wazungumzaji wanakuwa. Mzungumzaji yule yule anatumia lugha kwa namna mbalimbali katika hali tofauti na kwa madhumuni fulani. Wafanyakazi wa bandarini wanapokuwa katika muktadha rasmi ambao ni bandarini hutumia lugha kwa namna moja kwa kuwa hapa wana madhumuni sawa. Maoni haya yanaonyesha kwamba lugha hutumiwa kwa namna fulani kutegemea namuktadha wa mazungumzo. Muktadha wa mazungumzo ni mojawapo wa viamuzi vya lugha. Hali hiyo huwawezesha watu kuteua misamiati watakayoitumia ili pawepo na maafikiano baina ya msamiati na muktadha husika.

Hudson (1980:33) ametaja kanuni tatu ambazo hutawala mazungumzo nazo ni taaluma, ambayo hujishughulisha na madhumuni na mada ya mawasiliano, mtindo ambao hurejelea njia ya kutoa mawasiliano mfano, ni mazungumzo au maandishi, utaratibu hii inategemea uhusiano wa wazungumzaji. Katika kanuni ya kwanza, inaonyesha kuwa, mada ya mazungumzo huweza kusaidia katika kuteua msamiati unaokubalika katika taaluma husika. Zipo taaluma nyengine ambazo huhitaji mambo kusemwa waziwazi bila kutumia tasfida, na zingine humhitaji mzungumzaji kutumia

tasfida kuepuka kuwakera wasikilizaji. Stockwell (2002:7) rejista mbali mbali sharti zifungamanishwe na matarajio ya tamaduni ambazo zinamhitaji mtu kutumia lugha ya heshima hasa mbele ya hadhira. Hii inamaanisha kwamba muktadha ni kitu muhimu katika kutambua rejista na vile vile huwezesha mawasiliano kuendelea kwa kufuata mtindo fulani wa mazungumzo. Muktadha waweza kuwa wa msikitini, hospitalini, hotelini, kazini, shuleni au hata gerezani. Mazungumzo na uteuzi wa misamiati katika miktadha hii yatatofautiana. Rejista inaelekea kuwa muhimu hasa katika uteuzi wa rejista husika ili kuweza kuwiana na muktadha unaotumika. Rejista hizi zinatofautiana kwa kutegemea mada, muktadha, uhusiano na pia lengo la mzungumzaji. Mada wanayozungumza wanapokuwa wenyewe ni tofauti na wanapozungumza na tajiri aliyekuja kutoa taarifa kwamba ana mzigo wake anataka uchukuliwe. Hudson (1980:48) rejista ni matumizi ya lugha kutegemea na Muktadha. Hii inaonyesha kuwa, muktadha wa mazungumzo huathiri lugha inayotumiwa. Maoni haya yanaoana na ya Trudgill (2000:81) ambaye anasema kuwa lugha hutofautiana kutegemea tabia za wazungumzaji kama vile; tabaka, jamiilugha, jinsia lakini pia kutegemea na muktadha ambapo wazungumzaji wanakuepo.

Trudgill (2000:81) anaeleza rejista zina sifa tofauti za kimsamiati kama vile, matumizi ya maneno fulani fulani au kutumia maneno kwa maana fulani. Anaendelea kusema kuwa rejista ni mfano wa aina ya lugha inayotumiwa katika muktadha fulani. Kwa sababu hii, anasema katika jamii mtu mmoja anatumia lugha kwa namna mbali mbali katika hali tofauti kutokana na mazoea. Maoni haya ya mwanaisimu huyu yanaonyesha kuwa lugha hutumiwa kwa namna fulani kutegemea na muktadha wa mazungumzo.

Muktadha wa mazungumzo ni mojawapo wa viamuzi vya lugha. Muktadha waweza kuwa kanisani, msikittni, ofisni, shuleni, sokoni au hata gerezani. Halliday (1978:33) kuna kanuni tatu ambazo hutawala mazunguzo mfano taaluma, ambayo hujishughulisha na mada au malengo ya mawasiliano, Pili ni mtindo ambao hurejelea njia ya kutoa mawasiliano kama ni mazungumzo au maandishi na tatu ni Utaratibu ambao unategemea uhusiano wa wazuguzaji. Katika kanuni ya kwanza, mada ya mazungumzo huweza kusaidia katika kuteua msamiati ambao unakubalika katika taaluma husika. Kuna taaluma zingine ambazo huhitaji mambo kusemwa waziwazi bila kutumia tafisda, taaluma zingine humhitaji mzungumzaji kutumia tafisda ili asije akawakera wasikilizaji. Stockwell (2002:7) rejista mbali mbali sharti zifungamanishwe na matarajio ya tamaduni, tamaduni zinamuhitaji mtu kutumia lugha ya heshima hasa mbele ya hadhira. Hii ndio maana tunasema kuwa muktadha ni jambo muhimu la kuzingatia katika kutumia rejista. Kanuni ya pili ambayo ni mtindo, inaonyesha kuwa kuna tofauti wakati ambapo mtu anazungumza na wakati anapoandika. Mtu anapozungumza na washiriki wenzake katika kikundi atatateua msamiati unaoingiliana na mazungumzo yao na pia atakuwa akiifikiana na washiriki wenzake katika mazungumzo. Mtu huyo huyo wakati anapoandika, hamna athari kutoka kwa washiriki wenzake kwa hivyo atatumia lugha kama mtu binafsi Kanuni ya tatu, utaratibu, inaonyesha kuwa uhusiano wa wazungumzaji hutoa utaratibu wa mawasiliano. Chepe wa makuli anapozungumza na mwenzake watatumia lugha yao kama inavyotumiwa kuwatambulisha. Chepe huyo wa makuli anapozungumza na matajiri wa mizigo atabadilisha namna ya kuzungumza kwa namna tofauti. Utaratibu wa mawasiliano huelekezwa na uhusiano wa wazungumzaji. Kanuni hizi za Halliday ni muhimu kwetu tunapobainisha rejista ya makuli Katika rejista ya makuli wa

bandarini kanuni hizi zimesaidia katika kutambua ni kwa nini makuli wa bandarini huwasiliana kwa njia fulani wanapokuwa wenyewe na wanapokuwa na rmatajiri wengine katika sehemu ya bandarini. Rejista ya makuli wa bandarini inaweza tu kutambuliwa wanapokuwa katika muktadha wao wa kazi katika eneo la bandarini. Hii ni kwa sababu, katika eneo la bandarini, makuli wapo pale kwa shughuli maalumu ya upakuzi na ubebasji wa mizigo Kwa hivyo, rejista ya makuli wanapokuwa bandarini itatambuliwa kwa msamiati maalum. Msamiati huu maalum umetusaidia katika kuchanganua na kueleza rejista ya bandarini.

### **2.3 Mifano ya Rejista**

Pamoja na kueleza maana ya dhana mbali mbali katika utafiti huu ni vyema pia kuonyesha mifano ya rejista zilizoandikwa na wanaisimu mbali mbali ambazo zimetusaidia sana katika kufanikisha utafiti. Linda na Wareing (1999:143) wanaeleza kuhusu rejista ya kikundi cha watu wanaoishi mtaani huko New York kama ilivyoelezwa na William (2011). Hiki ni kikundi cha watu ambao wanaranda randa mitaani na hawana makao rasmi. Nchini Kenya wanajuilikana kwa jina la chokoraa, wote walitumia Kiingereza cha Wamarekani weusi kisicho sanifu. Wanaendelea kusema kwamba, katika kikundi hiki, kulikuwepo na vijana ambao walionekana kuwa na usemi zaidi kuliko wenzao, vijana hawa walichukuliwa na wenzao kuwa watu wa kimsingi katika kikundi hiki na kwa hivyo, usemi wao ndio ulionekana kuwa wa muhimu. Vijana hawa wa kimsingi waliweza kutumia lugha hii ya kienyeji kwa uthabiti zaidi pia alipata kuwa namna vijana hawa walihusishwa katika lugha ya kienyeji ndivyo walivyozidisha umahiri wao wa kuzungumza kwa kutumia Kiingereza cha Wamarekani weusi kisicho sanifu. Wanasema kuwa kitu



kilichotambulisha vijana katika kikundi hiki kimsingi ni lugha ambayo walitumia. Wale waliotumia lugha sanifu walichukuliwa kuwa vijana wa pembeni na si wa kiasili hasa. Hivyo, tunaona kuwa vijana hawa wa mitaani walipunguza mipaka yao ya usemi ili kuweza kutambuliwa kama vijana wa kimsingi katika kikundi hicho ingawa, vijana wa kimsingi hawakutumia Lugha sanifu, wale wa pembeni walitumia lugha hiyo hiyo ili kuweza kutambuliwa kama kijana wa kimsingi jambo ambalo lilikuwa ni la kifahari kwao. Utafiti huu ulionyesha kuwa, watu wa kikundi fulani hutumia lugha kwa namna moja licha ya kuwa wanavunja kanuni za lugha husika. Rejistta hii ya vijana wa mitaani ni muhimu kwetu. Tumezata kuona kuwa vijana hawa waliweza kupunguza mipaka ya kusemi baina yao ili kuweza kujitambulisha na kikundi husika. Makuli wa bandarini pia ni kikundi cha kijamii ambacho kinaweza kutambulishwa kwa kutumia aina ya lugha wanayoitumia.

Hata hivyo, utafiti wao unatofautiana na wetu kwa kuwa sisi tumechunguza todauti ya lugha ya makuli wa bandarini Zanzibar na lugha sanifu ya Kiswahili hivyo tunajikita katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Linda na Wareing (1999:144) pia wanaangazia utafiti uliofanywa na Eckert Penelope miaka thamanini iliyopita. Hapa walionyesha matumizi ya lugha huweza pia kuhusishwa na mitindo ya mavazi wanayoalia watu, mtindo wa kunyoa na aina ya muziki ambao watu wanapenda. Wanaonyesha kuwa, Penelope alichunguza wanafunzi wa shule ya upili viungani mwa mji wa Detroit. Penelope alipata kuwa katika shule ya upili, kulikuwa na makundi mawili ya kijamii: wanafunzi waliojikusha na shughuli mbalimbali za shule kama vile michezo na uigizaji, wangejiunga na vyo mbalimbali baada ya kukamilisha shule ya upili. Hawa walijitambulisha na kutambuliwa kwa jina la utani

“jocks”. Wanafunzi ambao hawakujihusisha na shughuli za aina hii, walijiunga na kazi za mikono huko mashinani, walitambuliwa na kujitambua kama “burnouts”. Wanafunzi waliovunja ungu; wavulana kwa wasichana walitambuliwa katika makundi haya. Hata hivyo, alisema wale wanafunzi ambao hawakuwa katika mojawapo ya makundi haya, walikuwa ni wana vuguvugu. Penelope kama alivyonukuliwa na wanaisimu hawa wawili anasema, tabia za kiisimu ziliweza kujitokeza kwa makundi haya. Wale wanafunzi waliojihusisha na shughuli mbalimbali za shule walitumia lafudhi ya tabaka la juu ilhali wale wengine walitumia lafudhi ya kienyeji.

Utafiti huu wa Penelope ni muhimu katika utafiti wetu. Katika nadharia ya maafikiano ya Giles, tunaelezwa kuwa ili watu binafsi waweze kutambulishwa na kikundi fulani cha kijamii, ni sharti kupunguza mipaka ya usemi baina yao. Katika utafiti wetu, tunachunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili ya makuli wa bandarini. Makuli wa bandarimi wana malengo ya kuhakikisha mizigo ya abiria na wafanya biashara wengine inabebwa, inatunzwa na kuwa salama kinyume na wanafunzi walio na maazimio tofauti. Wanafunzi wengine Kama anavyosema Penelope walijiunga na vyuo mbalimbali, wengine walifanya kazi za mikono baada ya masomo, lakini makuli wana kazi tayari, na wana Maazimio sawa. Kwa sababu hii, utafiti wetu umebainisha matumizi ya lugha ya Kiswahili ya makuli wa bandarini. Wardhaugh (1986:246) anasema kuwa, muktadha na utaratibu wa mawasiliano ni muhimu. Anatoa mfano wa rejista ya Malkia. Anasema kuwa ujumbe wa Malkia wakati wa Krismasi hukitwa katika muktadha na hutolewa kwa utaratibu washiriki wana hiari ya kubadilisha namna ya kuwasiliana kadri wanavyobadilisha shughuli waliyokuwa

wakifanya. Utafiti huu wa Wardhaugh una kipengele muhimu kwetu. Kipengele hiki ni hiari ya kubadilisha namna ya kuwasiliana na hata ujumbe unaotolewa pindi unapobadilisha mazingira. Utafiti wetu umechunguza namna makuli wa bandarini jinsi wanavyowasiliana wao wenyewe na namna wanavyowasiliana na matajiri wao. Hii ndio maana tunasema kuwa utafiti huu umetusaidia vizuri sana.

Spolsky (1998: 34) anachunguza rejista ya watu wa familia moja. Anajikita katika muktadha wa nyumbani. Anasema kuwa njia muhimu ya kupambanua hali ya kijamii ni kuziainisha katika sifa tatu bainishi: mahali, majukumu ya uhusiano na mada. Njia hizi tatu anazona kama kanuni. Kanuni mojawapo anasema kuwa ni nyumbani. Anaendelea kusema kuwa kanuni kwa kawaida hupewa jina kulingana na mahali au shughuli inayoendelea mahali hapo. Katika utafiti wake, mahali ni nyumbani. Majukumu ya uhusiano ya pahali hapo yalikusisha familia yaani, baba, mama, watoto na wageni wanaofika. Anasema kuwa katika muktadha wa nyumbani, mada zinazozungumziwa zinahusu shughuli za familia hiyo, haziwahusu wanajamii wengine, wala vyakula na vifaa vya nyumbani. Wanafamilia wanajua zaidi ya lugha moja, basi watatumia lugha tofauti kuelezea mambo tofauti, na katika majukumu ya uhusiano ya wanafamilia hutumia lugha tofauti ili kuonyesha uhusiano wao. Anatoa mfano wa mume na mke ambao anasema kuwa wanapowasiliana wanaweza kutumia lugha moja katika mazungumzo yao lakini baba anapozungumza na wanawe atatumie lugha tofauti. Hii ni kutokana na kuwa mume na mke wana uhusiano ulio tofauti na ule wa baina ya watoto na baba yao. Watoto na baba yao wana mipaka wanapozungumza na kwa hivyo hutumia lugha ambayo itakuwa mwafaka. Spolsky anasema kuwa kanuni nyingine ni kazi. Mahali panaweza kuwa kiwandani, afisi au

ghala. Majukumu ya uhusiano yanahusisha mkubwa wao, wafanyakazi, washiriki, Wenye mizigo, msimamizi, kastoma, na kadhalika. Mada itakayotawala inahusiana na kazi husika. Spolsky anaonyesha kuwa wakati wa mawasiliano baina ya watu mbalimbali wa jamii, wazungumzaji hutumia aina ya lugha ambayo ni mwafaka kulingana na uhusiano wao. Katika kanuni ya kazi pia anaonyesha kuwa uhusiano ni muhimu katika uteuzi wa lugha itakayotumika. Hii inaonyesha kuwa washiriki katika mazungumzo huchagua sajili watakayoitumia ili kuonyesha uhusiano wao. Maoni haya ya Spolsky ni muhimu kwetu. Kwa sababu katika utafiti wetu, tunachunguza rejista ya makuli wanapozungumza na wenye mizigo, waliokuja kutaka kufanyiwa kazi na wanapozungumza wao wenyewe.

Umoja katika kikundi cha kijamii ni tunu muhimu ya uhai wa mawasiliano baina ya wanakikundi hao ambayo ina athari katika rejista itakayotumika. Tunu hii inawezesha wanakikundi kuafikiana katika rejista wanayoitumia ili mwafaka kama ilivyo ule wa Rais wa Amerika wa kongamano la pamoja la kitaifa la kila mwaka. Wardhaugh anasema kuwa aina ya usemi unaotolewa huwa mwafaka katika hali fulani na huweza kuwa si mwafaka katika hali nyingine tofauti. Aina fulani ya mazungumzo huwa mwafaka katika muktadha fulani. Hata hivyo, kuwawezesha kufikia malengo yao. Kutokana na umoja huu unaodhihirika katika jamii ya wachukuzi wa bandarini, imetuwezesha kufanya uchunguzi ili kubainisha rejista yao. Rejista za wanaisimu hawa zimetuwezesha kuweka msingi wa utafiti wetu ambao unahusu rejista ya wachukuzi wa bandarini. Pamoja na hali hiyo katika kuchunguza rejista ya wachukuzi wa bandarini, matumizi ya lugha yao hayawezi kuepukwa.

#### **2.4 Rejista ya Makuli wa Bandarini Unguja**

Utafiti huu ulichunguza rejista ya wachukuzi wa bandarini kwa kujikita katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Mukhwana (1990:1) lugha haiwezi kutenganishwa na jamii kwa sababu mahusiano ya lugha ni mahusiano ya kijamii vilevile. Anaendelea kusema kwamba, kuchagua lugha fulani ili itumike mahali fulani kwa watu fulani hufanywa ili kuakisi muundo wa jamii husika ili kutosheleza mahitaji fulani ya kijamii. Kadri wanavyoendelea kuzungumza ndivyo wanaendelea kuafikiana. Hapa tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba, Makuli wakiwa ni kundi maalumu la kijamii wana mtindo wao maalumu wa kuwasiliana yaani rejista, ambapo ni tofauti na lugha sanifu ya Kiswahili katika maongezi yake.

Kamusi ya Kiswahili fasaha weanasema, Kuli ni mtu anayefanya kazi ya kubeba mizigo bandarini (Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) 2010.) Kutokana na wataalamu hao tunaweza kusema kwamba Kuli ni mtu yoyote anayefanyakazi ya kubeba mizigo ikiwa bandarini, sokoni, viwandani, maghalani pamoja na maeneo mengine ambako harakati za ubebaji wa mizigo zinaendeshwa kwa maslahi ya wanajamii wenyewe au Taifa kwa ujumla. Katika bandari ya Unguja, Kazi ya ukuli inafanywa na watu wenye rika tofauti na mara nyingi hufanywa na watu wazima wenye hekma na busara kubwa na aghalabu huwa wanaume kwa malengo na madhumuni yale yale ya kuendesha maisha yao kwa kutafuta kipato cha kihalali.

**Picha 1:** Makuli wakiwa katika harakati zao za kazi hapo bandarini huku wakitumia rejista zao mfano nipe nyuma, au ‘semile huko, semile huko’.



Makuli huku wakitumia rejita ya hodi hodi wakionekana wamebeba gunia la maharage kutoka katika boti ya mizigo inayotokea bara (Dar-salaam ).



Chanzo; bandari ya Zanzibar **Picha 2:**

**Picha 2:** Makuli wakipakuwa mzigo kutoka jahazini katika gati (bandari) ya majahazi iliopo mjini Unguja wakitumia ngazi ya mbao isiyo rasmin.



## **2.5 Kazi nyingine Zilizosaidia Utafiti Huu**

Habwe (1999) alichunguza lugha katika siasa za Tanzania na aligundua kwamba, hotuba za kisiasa zinakuwa na changamano kwa sababu mzungumzaji na hadhira wake wanahusika kwa nafasi kubwa katika kuendeleza hotuba hizo. Anaendelea kusema kwamba, hadhira huweza kuathirika katika mwelekeo chana au hasi kutokana na maudhui ya mada ya mzungumzaji katika hotuba inayotolewa. Anasisitiza kwamba muhitu katika mkutano wa kisiasa sharti aweze kutilia maanani matakwa ya hadhira wake na kinyume chake wafuasi wake wanaweza kuondoka mkutanoni. Naye Mang'eli (2008) alichunguza maana ya dhana ya Majimbo na Mabadiliko Kama zilivyotumiwa katika uchaguzi wa kitaifa wa mwaka 2007 nchini Kenya. Kwa kutumia nadharia ya Uhusiano Mangel (TYA)

alichunguza namna lugha ilivyotumika katika kupata nafasi, dhana hizi ziliweza kutumiwa na vyama vya siasa nya ODM na PNU vilivyokuwa vikiwania viti mbalimbali. Alichunguza namna dhana hizi ziliweza kuwasilishwa kwa wapiga kura na athari iliyotokana na dhana hizi. Aidha aligunduwa kwamba wapiga kura waliweza kuathiriwa kutokana na maudhui ya dhana hizi kulingana na rejista iliyotumika na hivyo wafuasi walijigawa katika makundi hayo mawili makuu kwa kukubali au kukataa kuunga mkono sehemu moja wapo. Mfano, wafuasi wa ODM waliunga mkono dhana hizi ilhali wale wa PNU walipinga dhana hizi. . Utafiti wake umetufaa katika kuelewa kwamba kila kundi lina aina yake ya kuwasiliana na ni tofauti na kundi jengine la kijamii kama lilivyo kundi la makuli wa bandarini unguja. Kwa sababu hii, wanasisa hutumia rejista maalumu ambayo ina ushawishi ndani yake ili kuvuta mawazo ya hadhira husika. Utafiti wetu unalingana lakini hauko sawa na watafiti niliowataja, sisi tulichunguza rejista ya makuli wa bandarini unguja ambao na wao hutumia aina maalumu ya rejista katika eneo lao la kazi kwa dhamira ya kuwalainisha matajiri wao ili wakubaliane na matakwa yao hasa katika mapatano ya ujira wa kazi wanazozifanya.

Hata hivyo, utafiti huu umekuwa wa manufaa kwetu hasa kwa kuwa tulichunguza athari za lugha ya makuli wa bandari ya Malindi iliopo mjini Unguja kwa watumiaji wengine wa bandari hiyo mfano abiria wanaoingia na kutoka kupitia bandari hiyo. Njenga (2008) alichunguza mtazamo wa Myers Scotton (1993) ambao ulijikita katika kuchunguza ikiwa uhusiano wa kijamii huweza kuchochea kubadili msimbo kutoka kwa lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Alijikita katika mazungumzo ya Vipindi vya radio vya ‘Easy Breakfast’, ‘Easy Connection’na Easy Jam’. Hivi ni vipindi



ambavyo watu hutoa mchango wao. Matokeo yake yanaonyesha kuwa baadhi ya kanuni za mtazamo huu wa Myers Scotton ziliweza kujitokeza katika data yake na kwa hivyo kuna ubia unaojitokeza. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa kuwa kuna ufumbuzi kuwa rejista ya makuli wa bandari ya Malindi Unguja husheheni kuchanganya ndimi na kubadili msimbo. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na wetu kwa kuwa tunatumia nadharia tofauti.

Fairclough (1989) anazungumzia kuhusu umaanisho baina ya lugha na asasi za kijamii katika masuala ya kisiasa na miundo ya kijamii. Ameibuka na athari za kiisimu ambazo hutokana na wasikilizaji wanaposikiza matangazo maalumu, biashara, siasa na semi katika vyombo vya habari. Kwa kuzungumzia lugha, anasema kuwa ni matokeo ya uhusiano wa mamlaka na kupigania mamlaka. Anaona mambo haya kama uhalisi wa kawaida ambao huchukulia kuwa mamlaka na mfumo wa ngazi kama vitu halisi. Anatoa mfano wa chukulizi hizi ambao ni itikadi. Anasema kuwa itikadi huhusishwa na mamlaka, kwa sababu, uhalisi wa chukulizi za itikadi hufungamanishwa na mapatano kutegemea na uhusiano wa mamlaka ambao huleta mapatano hayo. Anasema kuwa itikadi fulani huhalalisha uhusiano uliopo wa kijamii na tofauti za mamlaka. Kulingana naye, hii husababishwa na mazoea na tabia zinazofanana ambazo huwafanya watu kuchukulia mahusiano haya kimzaha. Fairclough anaendelea kusema kuwa itikadi huhusishwa na lugha.

Maoni ya Fairclough (TYA) ni muhimu katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu, makuli wa bandarimi hutumia lugha kwa namna moja kutokana na uhusiano wao na pia kutokana na uhalisi wa kazi yao ambayo huwapa mamlaka. Maoni haya yametusaikia katika kuchunguza rejista ya makuli wa bandari ya malindi iliopo mjini

Unguja ambayo inawatambulisha wao kama kikundi cha kiisimu. Tumechunguza Kama mamlaka walio nayo makuli wa bandarini ambayo huwafanya kuzungumza kwa namna fulani. Mamlaka haya huathiri jamii husika, kwa kuwa makuli wa bandarini hutumia lugha kwa namna ya kipekee kwa kuwa wana mamlaka fulani ambayo Fairclough anayaita maafikiano 'asilia.' Maoni ya Fairclough yametusaikia katika kutambua rejista ya makuli wa bandari ya Malindi iliopo mjini Unguja kwa kujikita katika muktadha wao wa kazi. Linda na Wareing (1999: 144) pia wanaangazia utafiti uliofanywa na Eckert Penelope miaka ya thamanini iliyopita.

Hapa wanaonyesha kuwa matumizi ya lugha huweza pia kuhusishwa na mitindo ya mavazi inayotumiwa na wanajamii, mtindo wa kunyoa na aina ya muziki ambao watu wanapenda. Wanaonyesha kuwa, Penelope alichunguza wanafunzi wa shule ya upili viungani mwa mji wa Detroit. Penelope alipata kuwa katika shule ya upili, kulikuwa na makundi mawili ya kijamii: wanafunzi waliojihusisha na shughuli mbalimbali za shule kama vile michezo na uigizaji, na kujiunga na vyo mbalimbali baada ya kukamilisha shule ya upili. Hawa walijitambulisha na kutambuliwa kwa jina la utani jocks. Wanafunzi ambao hawakujihusisha na shughuli za aina hii, walijiunga na kazi za mikono huko mashinani walitambuliwa na kujitambua kama burnouts. Wanafunzi waliovunja ungo; wavulana kwa wasichana walitambuliwa katika makundi haya. Hata hivyo, anasema kwamba kuna wale wanafunzi ambao hawakuwa katika mojawapo wa makundi haya. Hawa walikuwa ni kundi la vuguvugu. Penelope Kama alivyonukuliwa na wanaisimu hawa wawili anasema kwamba tabia za kiisimu ziliweza kujitokeza kwa makundi haya. Wale wanafunzi

waliojihusisha na shughuli mbalimbali za shule walitumia lafudhi ya tabaka la juu ilhali wale wengine walitumia lafudhi ya kienyeji.

Utafiti wa Penelope ni muhimu kwetu. Katika nadharia ya maafikiano ya Giles, tunaelezwa kuwa ili watu binafsi waweze kutambuliwa kwamba ni kikundi fulani cha kijamii, ni sharti kupunguza mipaka ya usemi baina yao. Hivyo katika utafiti wetu, tulichunguza matumizi ya rejesta ya kikundi maalumu cha makuli wa bandarini Unguja na kuangalia maana ya rejesta kwa kulinganisha maana hiyo na lugha ya Kiswahili. Makuli wa bandarini wana malengo yao ya kubeba na kupakia mizigo na pia kuwasaidia abiria wenye mizigo ili wasipate usumbufu wowote wakiwa safarini kupitia bandari ya unguja ni kinyume na wanafunzi walio na maazimio ya kielimu zaidi kwa kujilinganisha na wanafunzi wengine katika vyuo na shule mbali mbali kakama anavyosema mtafiti Penelope kwamba wanafunzi baada ya kuhitimu walifanya kazi za ujuzi za kutumia mikono lakini makuli wa bandarini kazi zao zipo tayari siku zote. Kwa sababu hii, utafiti wetu unabainisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa muktadha wa bandarini Unguja.

Wardhaugh (1986:246) anasema kuwa, muktadha na utaratibu wa mawasiliano ni muhimu. Anatoa mfano wa rejesta ya Malkia, anasema kuwa ujumbe wa Malkia wakati wa Krismasi hukitwa katika muktadha ya kimalkia na hutolewa kwa utaratibu mwafaka kama ilivyo ule wa Rais wa Amerika katika kongamano la pamoja la kitaifa la kila mwaka. Wardhaugh (TYA) anasema kuwa aina ya usemi unaotolewa unakuwa mwafaka katika hali moja na kwa hali nyengine ulikuwa si mwafaka. Utafiti wa Wardhaugh una kipengele muhimu cha uhiari ambacho hubadilisha namna ya kuwasiliana na hata ujumbe unaotolewa pindi unapobadilisha mazingira. Ni sawa

na utafiti wetu unaochunguza namna makuli wa bandarini wanavyotumia rejista wakati wa kuwasiliana na wenyewe na namna wanavyowasiliana na wateja wao (wasafiri). Spolsky (1998: 34) anachunguza rejista ya watu wa familia moja na anajikita katika muktadha wa nyumbani. Anasema kuwa njia muhimu ya kupambanua hali ya kijamii ni kuziainisha katika sifa tatu bainishi yaani, mahali, majukumu ya uhusiano na mada. Njia hizi tatu anaziona kama kanuni muhimu katika mwasiliano. Kanuni ya mahali ambayo ni nyumbani inahusishwa na familia yaani, baba, mama, watoto na wageni wanaofika. Anasema kuwa katika muktadha wa nyumbani, mada zinazozungumzwa zinahusu shughuli za familia hiyo, na haziwahusu wanajamii wengine, vyakula na vifaa vya nyumbani. Aina fulani ya mazungumzo ni mwafaka katika kanuni hii ya nyumbani. Katika familia ambapo wanafamilia wanajua zaidi ya lugha moja, basi walitumia lugha tofauti kuelezea mambo tofauti yanayohusu majukumu ya uhusiano wao, wanafamilia hutumia lugha tofauti kuonyesha uhusiano wao. Anatoa mfano wa mume na mke ambao wanapowasiliana wanaweza kutumia lugha moja katika mazungumzo yao lakini baba anapozungumza na wanawe alitumia lugha tofauti. Hii ni kutokana na kuwa mume na mke wana uhusiano ulio tofauti na ule wa baina ya watoto na baba yao. Watoto na baba yao wana lugha ambayo itakuwa na rejista maalumu iliyojaa nidhamu na heshima ya hali ya juu.

Spolsky (TYA) anasema kuwa kanuni nyingine ni kazi. Mahali panaweza kuwa kiwandani, ofisini aukwenye maghala. Majukumu ya uhusiano yanahusisha; mkubwa wao, wafanyakazi, washiriki, wateja, msimamizi, mteja, na kadhalika. Mada itakayotawala inahusiana na kazi husika. Spolsky anaonyesha kuwa wakati wa

mawasiliano baina ya watu mbalimbali wa jamii, wazungumzaji hutumia aina ya lugha ambayo ni mwafaka kulingana na uhusiano wao. Katika kanuni ya kazi pia anaonyesha kuwa uhusiano ni muhimu katika uteuzi wa lugha itakayotumika. Hii inaonyesha kuwa washiriki katika mazungumzo huchagua rejista watakayoitumia ili kuonyesha uhusiano wao. Maoni haya ya Spolsky ni muhimu kwetu. Kwa sababu katika utafiti wetu, tunachunguza rejista ya wafanyakazi wa bandarini (makuli) wanapozungumza na wateja wao wenye mzigo au wao wenyewe. Kinachojitokeza hapa ni ukweli kwamba uhusiano huelekeza aina ya rejista itakayotumika katika mawasiliano. Makuli wa bandarini wanapozungumza na wenzao walitumia rejista tofauti na wanapozungumza na wasafiri au watu wengine. Katika kutekeleza kazi zao vizuri na kwa ufanisi wa hali ya juu, makuli kwa upande wao walizingatia umoja na ushirikiano ulio thabiti bila kujali rangi au kabila au eneo la mtu analotoka. Umoja katika kikundi cha kijamii ni silaha muhimu ambayo huleta taathira ya maendeleo ya lugha na kijamii. Jambo linalojitokeza ni kwamba muktadha wa mazungumzo na uhusiano wa washiriki katika mazungumzo ni mambo muhimu katika uteuzi wa rejista itakayotumika. Muktadha ni muhimu kwa sababu huelekeza mada zitakazozungumziwa. Katika muktadha wa eneo la bandarini mada zitahusiana na shughuli za utekelezaji wa majukumu yao. Bright, W. (1992) alichunguza rejista ya lugha ya kiingereza nchini Marekani na aligundua kwanba, lugha kingereza ilitumika katika makundi matatu makubwa, ambayo ni Kiingereza cha visiwa vya Uingereza, Kiingereza cha Amerika ya kaskazini na Kiingereza cha Australia na kila kundi kuwa na rejista yake maalumu ambayo ni tofauti na kundi jengine. Tofauti hizo za mawasiliano ziliweza kusababisha kuwepo kwa matabaka, makundi yenye tofauti ya umri, jinsi cheo na hadhi. Rejista zinazotokana na jinsi, umri, matabaka na hadhi ya

wazungumzaji mfano wanawake hutumia neno *shost na* wanume hutumia neno *msela* wote wakiwa na maana ya rafiki katika Kiswahili sanifu. Hali hii pia ilisaidia sana utafiti wetu kwa kuona rejista nazo husababisha kuwepo kwa makundi ya utabaka, hivyo ushirikiano ni jambo jema.

Prasad (2012) katika utafiti wake wa lugha za Kichina alibaini kwamba watu wa China wanazungumza tofauti kutoka eneo moja na jingine na kila eneo huwa na kundi lenye rejista inayowatambulisha ambayo ni tofauti na kundi jingine. Mtindo wa lugha unaotumika hapo ndio utambulisho wao na kati yao hakuna mfanano wa aina yeyote. Kwa mfano mtindo wa lugha inaozungumzwa Cantonese ni tofauti na ule unaozungumzwa na watu wa Peking na Yunnanese. Licha ya kwamba msamiati wote unatokana na jamii moja. Hivyo, utafiti huu nao ulimsaidia sana mtafiti kuona mitindo ya utumiaji wa lugha katika kupashana habari kutoka jamii moja na nyingie unavyotofautiana. Hii ni sawa na rejista ya makundi ya watu wa hotelini na watu walioko mazikoni. Hivyo, Mtafiti wa utafiti huu alitumia kuona tofauti ya mazungumzo ya kundi la wafanyakazi wa bandari ya Malindi mjini Unguja na makundi mengine kama kundi la vyuo, makundi ya msibani, kanisani, msikitini na makundi mengine ya kijamii.

Katika Bara la Afrika lenye wakazi wengi wenye makabila na lugha tofauti Bright (1992) anasema, waafrika pamoja na kutumia lugha nyingi zenye lahaja tofauti wanatofautiana katika misimbo yao katika matamshi. Kwa mfano, alichunguza lugha ya zulu ya Afrika ya kusini inayotumiwa na wazungumzaji wasiopungua milioni kumi kama lugha yao ya awali na watu wasiopungua milioni kumi na sita wanaoitumia kama lugha yao ya pili huko Afrika ya kusini. Bright (TYA),

ameendelea kusema kwamba, lugha ya Zulu ina uwiano mkubwa na makundi yanayozungumza Lugha zilizo chini ya kundi la Lugha za Nguni ambazo ni Xhosa na Swazi lakini kila kundi lina rejista yake ambayo ndio utambulisho wao ambao huwa ni tofauti na makundi mengine. Makundi ya maeneo ya Zulu-Natal, Mpumalanga, Johannesburg na eneo la Kaskazini ya Free state huko nchini Afrika ya kusini, hutofautiana kimtindo namna ya kupashana habari kwao. Kutokana na ukweli huo mtafiti ameona kwamba utofauti wa eneo huko Afrika ya kusini ni sawa na eneo maalumu la watumiaji wa lugha kama lilivyo eneo maalumu la bandarini Unguja ambapo mtafiti amejikita katika kufanya utafiti katika kuchunguza mtindo au rejista ya makuli wa bandari ya malindi iliyopo mjini Unguja.

## **2.6 Mkabala wa Kinadharia**

Katika sehemu hii tumeelezea iliyotumika katika utafiti huu kama ifuatavyo:

### **2.6.1 Dhana ya Nadharia**

Massamba (2004) anatoa maana ya nadharia kwa kusema ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimaielezo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielezo cha kuelezea jambo. Naye Sengo (3009) anasema nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, muongozo mkuu wa mtu au wa jamii na pahala na wakati. Katika kufikia malengo ya utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia tatu tofauti ambazo ni nadharia ya isimujamii ya msimbo, nadharia ya maafikiano na nadharia ya vitendo usemi. Nadharia hizi zimekuwa ni kielelezo muhimu katika kufikia ufumbuzi wa tatizo la utafiti huu na kuweza kutoa jibu linalohusu rejista ya makuli wa bandarini Unguja na lugha ya Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu, tumechunguza mambo kadha yanayohusiana na makuli wa bandarini. Kwa sababu hii, nadharia hizi

zitakuwa ni dira au muongozo wa kufikia majawabu juu ya maswali yetu ya utafiti kama yalivyojitokeza hapo kabla kama ifuatavyo:-

### **2.6.2 Nadharia ya Isimujamii ya Misimbo (Bernstein 1964)**

Nadharia hii ya isimujamii inahusu misimbo ambayo hurejelea upangaji wa kanuni ambazo hutumiwa na watu wa kikundi fulani cha jamii wakati wa kutumia lugha ile ile kwa ajili ya mawasiliano. Kwa sababu hii, mahusiano ya watu huweza kuathiri aina ya lugha na matumizi ya lugha katika kikundi hicho. Nadharia hii inahusishwa na Basil Bernstein (1964). Bernstein anaeleza kwamba, matumizi ya lugha ya kila siku yanaakisi na kuonyesha hali halisi ya chukulizi kuhusu utambulisho wa kikundi fulani. Kikundi husika huweza kuathiri matumizi ya lugha ya mtu binafsi ili aweze kutambulika katika kikundi hicho. Bernstein anasema kuwa lugha ni kitu cha kimsingi katika kuanzisha na kuimarisha namna ya kufikiri, hisia na tabia ambazo huhusishwa na makundi ya kijamii. Bernstein, anadai kwamba sura za lugha inayozungumzwa na huku watu wakiwa wanafundishwa huwafanya wawe na mahusiano fulani maalum yanayohusishwa na mazingira yao. Hii inaonyesha kuwa lugha anayotumia mtu huweza kutambulisha nafasi yake katika jamii. Bernstein anachukulia lugha kama kaida zilizoidhinishwa ambapo misimbo ya usemi hutumika. Misimbo hii ya usemi hutokana na mfumo wa mahusiano ya kijamii. Kulingana naye, muundo wa uhusiano wa kijamii huwa maalum kutokana na kinachosemwa, yaani wapi na namna kinavyosemwa. Katika mtazamo wa isimujamii, ni wazi kuwa watu huweza kujua majukumu yao kupitia mawasiliano ambapo majukumu hayo ni ule uelewa wa pamoja wa kikundi fulani. Bernstein anazungumzia misimbo miwili; msimbo pana na msimbo finyu. Kiisimu, msimbo



pana unahusu kuwepo kwa mawanda mapana katika uteuzi na ubashiri wa vipengele vinavyozungumziwa na kwa hivyo uwezekano wa kubashiri huwa umepunguzwa. Katika msimbo pana kila kitu husemwa waziwazi ili kila mtu aweze kuelewa ilhali msimbo finyu mawanda ni finyu na uwezekano wa watu walio nje ya kundi hilo kuelewa kinachosemwa huwa umepunguzwa. Msimbo finyu huleta hali ya umoja. Msimbo huu huwa umebanwa na wanaoelewa huwa ni wale tu walio katika kikundi fulani husika. Huwafanya watumiaji wengine wa lugha kuhisi kuwa hii ni lugha ya watu wa kikundi maalum. Msimbo finyu hutenga watu wasio katika kundi hilo na ni njia moja ya kuhifadhi siri za kundi la makuli. Nadharia ya isimujamii ya misimbo imetuwezesha kutambua ikiwa makuli wa bandarini hutumia msimbo finyu ambao hulenga utoaji wa maana kwa kutumia maneno ambayo yanaoana na muktadha wa mazungumzo na ambayo yanaeleweka na watu wa kikundi hicho mahsusi au wanatumia msimbo pana ili kila mtu aweze kuelewa. Bernstein (1964) anahitimisha kwa kusema kadri mtu anavyojifunza amaweza kuhusisha tabia yake na msimbo wa kiisimu, ambao ndio dhihirisho la majukumu na taratibu mbalimbali za uhusiano hujitokeza. Ni kupitia kwa msimbo maalum wa kiisimu ndio uhusiano hujengeka, uzoefu wa muundo fulani ndio huthibiti utambulisho wa kikundi hicho. Msimbo finyu na msimbo pana hutambulisha maana ya mawasiliano ya kundi maalumu la makuli wenyewe na kuonyesha utafauti wa kimaana na watumiaji wengine wa lugha ya Kiswahili sanifu. Nadharia hii imekuwa ni muhimu na muongozo katika kufikia jibu la swali la kwanza linalotaka kujua tofauti ya kimaana kati ya rejista ya makuli wa bandarini unguja na lugha sanifu ya kiswahili, kwani imetuonyesha maana ya wazi kwa kutumia msimbo pana, na maana iliyojificha kwa kutumia msimbo finyu. Maana hizo hazina tofauti kubwa na lugha ya Kiswahili sanifu.

Hivyo, nadharia hii imeweza kuwa ni dira katika kufikia lengo mahasusi la kwanza la utafiti huu. Pamoja na ubora wa nadharia hii wa kutowa muongozo juu ya kufikia majibu ya swali la kwanza lakini bado haijatosheleza kujibu maswali yote katika utafiti huu, mfano bado haijaonyesha kwa vipi au kwa namna gani rejista ya nakuli iliibuka na kuwa ni lugha ya kundi maalum kiojamii kama ilivyo hivi sasa. hivyo nadharia nyengine inahitajika katika kutoa muongozo na kueleza kwa namna gani lugha huibuka katika makundi kama hayo na kuibuwa muundo maalumu wa mawasiliano ambao utawatambulisha kama ni kundi maalum, u la kijamii.

### **2.6.3 Nadharia ya Maafikiano ya Giles (1979)**

Nadharia ya maafikiano ni moja kati ya nadharia muhimu katika utafiti wetu ambayo iliasisiwa na mwanaisimu Giles (1979), yeye nasema, watu wanapoingiliana huweza kubadili usemi unaotokana na sauti pamoja na ishara zao ili kuafikiana na wengine katika kikundi maalumu cha kijamii chenye kutumia muktadha wa aina moja na kusababisha mabadiliko fulani ndani ya wana kikundi husika. Kwa mfano mabadiliko hayo hutokea kwa watu binafsi ambao wanaungana na watumiaji wengine wa bandari ya Malindi iliopo mjini Unguja ili kuweza kuafikiana na makuli wa bandarini. Nadharia hii inahusisha sababu za watu binafsi kutoweza kuwasiliana na kuzungumza katika mipaka ya kijamii baina yao na washiriki wengine katika mazungumzo kupitia kwa wanayoyasema na ishara zao za kimawasiliano. Haijijhusishi tu na uhusiano baina ya muktadha wa utambulisho, lakini pia, huhusishwa na mahusiano baina ya kikundi fulani na mtu binafsi kwa kuangazia vipengele vinavyopelekea kuwepo kwa maafikiano. Msingi wa nadharia hii ni, mtu binafsi kupunguza tofauti za usemi baina yake na kundi analohusishwa nalo.

Mwanaisimu Giles (TYA) katika nadharia hii anasema utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii ugha ambayo nadharia hii inaviekeza kwa upana na kutupa mwelekeo mzuri wa kufanikisha utafiti wetu. Nadharia hii jumuishi inazingatia fasili ya jamii lugha inayosema jamii inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambuwa wenyewe. Giles (TYA) anatoa maana ya utambulisho kwa kusema kila jamii lugha yenyewe haina budi kujitambua kuwa iko tofauti na jamii lugha nyengine katika maswali ya msingi kama utamaduni,, mila, kazi, desturi, imani, chakula, mavazi, uchumi au siasa Makuli wa bandarini hufuata mtindo mmoja wa kutumia lugha, kwa sababu hii, tumeweza kuelewa sababu inayowawezesha kutumia lugha kwa namna moja kwa kutumia nadharia ya maafikiano. Kupunguza tofauti za matumizi ya lugha huwa njia moja ya kujitambulisha na kundi hilo husika. Maafikano hutegemea hali na kiwango cha kiisimu ambacho kinawezesha maafikiano. Watu wanaopenda kutambulishwa na kundi fulani huweza kuafikiana na washiriki wa kundi hilo kwa urahisi kuliko wale wasiopenda kundi hilo, hasa ikiwa mtu amelazimishwa kujiunga na kundi fulani kikazi, huchukua muda kutumia lugha na kuwa na tabia zilizo sawa na washiriki wa kundi hilo.

Hata hivyo, hatuna uhakika ikiwa mtu hulazimika kuwasiliana kama washiriki wakundi lake, au hilo ni jambo ambalo huja tu kwa hiari ili kupunguza tofauti baina yao. Giles anaendelea kusema kuwa, ili kuweza kuafikiana na watu wa kundi husika, watu huwa na uwezo wa kiisimu ambao huwawezesha kuwa kama washiriki wengine wa kundi hilo. Nadharia hii inashughulika na vipengele viwili, navyo ni: Uhusiano baina ya lugha, muktadha na utambulisho. Masuala ya kikundi na ya mtu binafsi

ambayo hupelekea uwepo wa maafikiano na vilevile namna miktadha ya kimakro na kimaikro inavyoathiri tabia za kiusemi. Mambo haya ni muhimu katika kuchunguza rejista ya makuli wa bandarini kwa kuwa yametusaidia kuelewa maafikiano baina ya makuli wa bandarini hasa wanapokuwa katika mazingira yao ya kazi katika eneo lao la bandarini. Giles anatia msisitizo dhana mbili, ambayo ni mwingiliano na ulahajishaji. Muingiliano ni msingi ambao unahusu hali ambapo watu huendelea kuafikana kwa namna ya kuzungumza kwa ishara ili kupunguza tofauti baina yao. Kwamba mtu huacha vile alivyozea kuzungumza na kufuata mtindo wa washiriki wengine katika kikundi hicho.

Na jambo la pili ni Ulahajishaji: hii ni hali ya kuongezeka kwa tofauti katika lugha hadi kufikia hatua ya kutokea lahaja, (TUKI 1990: 21). Kulingana na Giles, ulahajishaji ni hali ambapo mtu binafsi hutilia mkazo tofauti za kiusemi na kiishara baina yake na washiriki wengine wa kundi hilo. Hii inaonyesha kuwa hataki kuzungumza au kuwasiliana kama wanaovyowasiliana washiriki wengine wa kikundi hicho. Kwa kufanya hivi, mtu huyo hawezi kutambulishwa na kundi hilo kwa kuwa hamna maafikiano baina yake nawenzake. Katika utafiti wetu, tumejikita katika dhana ya mwingiliano kwa sababu, kadri mtu binafsi anavyojihusisha na mwingiano katika kundi fulani ndivyo maafikiano baina yake na washiriki wengine huongezeka na hii huashiria kuwa amekubali kazi anayoifanya na kukubali kuwa katika kikundi hicho. Inaaminika kuwa makuli wa bandarini kama kikundi cha kijamii huwa na mtindommoja wa kuzungumza. Kwa hivyo, yule anayejiunga nao hana budi kuafikiana na washiriki wengine kama njia ya kujitambulisha na makuli wengine. Ulahajishaji pia umekuwa muhimu kwetu hasa tunapobainisha mazungumzo baina

ya makuli wa bansarini na matajiri wao. Wamiliki wa mizigo ( matajiri ) hutumia lugha kwa namna walivyo zoea na ndio maana utampata akizungumza kwa lugha sanifu kinyume na ilivyo kwa msafiri wa kawaida anayetumia bandari hiyo ambaye anaweza kuchanganya ndimi.

Nadharia ya maafikiano imekuwa ni muhimu sana katika utafiti huu unaohusu rejista ya makuli wa bandari ya Malindi iliopo mjini unguja kama ni kundi maalumu la kijamii kwa sababu imesaidia kupata muongozo imara wa kujibu swali la pili ambalo lilikwenda sanbanba na lengo mahasusi la pili lililotaka kubainisha sababu za kuibuka rejista ya makuli wa bandarini unguja. Makuli ni watu wanaotoka katika jamii mbali mbali, lakini kwa sababu ya maingiliao yao na kuzaa maafikiano wameweza kuibuwa mtindo wao maalumu wa mawasiliano ambao ni tofauti na makundi mengine mfano makundi ya vyuoni, mahakamani ,msibani, kanisani msikitini na sehemu nyengine. Kutokana na hali hiyo tunahitimisha kwa kusema kwamba nadharia ya maafikiano ya Giles imekuwa ni kielelezo kizuri cha kufikia majibu ya lengo letu mahasusi la pili la kubainisha sababu za kuibuka rejista ya makuli wa bandarini.

#### **2.6.4 Nadharia ya Vitendo Usemi (Austin na Searle 1975)**

Nadharia za Bernstein ya isimujamii ya msimbo na ile Giles ya maafikiano hazitoshi katika kuchanganua lugha ya makuli wa bandarini kutokana na kasoro zilizopo katika nadharia hizo hivyo nadharia nyengine inahitajika katika kukamilisha malengo ya utafiti huu. Nadharia ya vitendo usemi iliyoasisiwa na mwanaisimu Austin na Searle (1975) ilikuwa ni tiba muwafaka katika kukamilisha malengo ya utafiti huu kwa kiwango kikubwa. Nadharia hii inahusu mfuatano wa kauli za kusemwa na

viendo wakati ya mawasiliano ya makundi ya watu kama ilivyo kwa makuli na wateja wao hapo bandarini unguja. Kwa mfano, Makuli wanapobeba mizigo hutoa kauli kwa wateja wao kwa kuwaiita, **mzee/kaka/dada**,“**toasasa**”. Matajiri wanaobebewa mizigo na wao huuliza kwa kutaka kuelewa zaidi kiasi gani? hujibiwa wewe toa tu, na hatimaye kitendo cha kutoa ujira hufanyika kutokana na usemi uliotolewa kulingana na uzito wa kazi iliyofanyika. Utendaji huu wa vitendo unaonyesha namna, maana na vitendo vinavyoleta uhusiano katika lugha kama ilivyonukuliwa na Schiffrin (1994: 59): Kwa kusema, mawasiliano hutegemea mambo yanayojulikana kuhusiana na jina na vitendo usemi; Mzungumzaji na mzungumziwa huwa na uzoefu sawa wa namna ya kutambua na kubainisha usemi kama kitendo fulani, ma kipengele cha lugha kinachotolewa na hufasiriwa kulingana na kanuni za vijenzi. Schiffrin anasema kuwa kuwasiliana kwa kutumia vitendo, hutegemea uelewa wa makundi yote mawili. Anayeambiwa atende jambo fulani, hilitenda kwa kuwa anaelewa alichambiwa afanye. Makuli wa bandarini huwaambia matajiri wao kufanya vitendo wanavyovijua au walivyozoea kwa mfano, Kuli anaweza kumwambia tajiri wake nipe “**Hoko**” yangu. Kwa sababu mwenye mizigo huwa ana uzoefu juu ya kifaa hicho kinachosaidia kubebea mizigo na kuupeleka juu ya bega huwa anafanya bila ya kusita Hii ina maana kwamba katika matumizi ya lugha kuna vitendo fulani vinavyotendwa. Vitendo hivi hutendeka katika muktadha maalumu. Naye Austin anasema, kila hatua ya lugha inatenda kitendo fulani, hii ina maana kwamba, katika matumizi sahihi ya lugha, vitendo hivi huwa ni vingi mno. Vitendo vya Lokusheni, vitendo hivi anavifafanua kuwa ni utoaji wa sauti na maneno yenye maana, kuanzia safu ya fonolojia hadi maana. Searle (1975), anasema kwamba kipengele cha kimsingi katika mawasiliano ni vitendo

usemi ambavyo anaviona kuwa ni kiini cha utafiti wa maana ya lugha na mawasiliano. Katika utafiti huu, nadharia ya vitendo usemi, imesaidia katika kuelewa masharti ya kutoa usemi na kuelewa usemi kama kitendo cha kiisimu. Hii imetusaidia katika kuchunguza usemi unaotumiwa na makuli wa bandarini kwa kuangalia namna vitendo hivyo vinavyohusiana na kanuni na masharti ya vitendo fulani; kuchunguza namna usemi unavyopelekea kutokea kwa vitendo nahivyo kujaribu kuelewa kwa nini hutumiwa na makuli wa bandarini au sehemu nyingine inayobebwa mizigo kama sokoni. Nadharia ya vitendo usemi imetuwezesha kutambua hali zinazopelekea utoaji wa usemi kama kitendo cha kiisimu. Kwa hivyo nadharia hii imekuwa muhimu katika kuchambua usemi wa rejista ya makuli wa bandarini, na imekuwa muhimu katika kujibu sawli la tatu ambalo linakwenda sanbanba na lengo mahasusi la tatu ambalo limechunguza athari zinazoweza kujitokeza kwa watu wengine wanaotumia bandari ya unguja mfano wasafiri kutokana na matumizi ya rejista hiyo. Katika nadharia ya vitendo usemi, lugha hutumiwa katika kutenda vitendo na imesaidia kuonyesha athari mbali mbali zinazotokana na lugha ya makuli kwa watumiaji wengine. Kwa mfano moja kati ya athari kubwa inayoonekana ni utii wa amri, na heshima nzuri, hii inatokana na kwamba mara tu usemi wa kutenda jambo ukitolewa na kiongozi wa makuli (chepe) kinachofuata ni kitendo vya kutekeleza amri hiyo, mfano pandisha mzigo unapandishwa kwenye rosa (ghalani ) haraka iwezekanavyo.

Aidha, athari nyengine inayojitokeza ni ujengaji wa dhana potofu au isiyo sahihi kwa baadhi ya wapita njia wa bandarini kutokana na usemi unaotolewa na makuli wakatri wa kazi. Mfano ulipotolewa usemi au amri ya naomba nyuma wakati kuli akiwa na

mzigo wengine walifikiri kuli anatukana au anapenda maneno ya matusi jambo ambalo sio sahihi kulingana na uchunguzi wa mtafiti wa utafiti huu. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kwamba nadharia ya vitendo usemi imekuwa ni muongozo mzuri wa kufikia maamuzi ya kuona athari mbali mbali zinazojitokeza wakati wa utumiaji wa rejiaata ya makuli wa bandarini iliopo mjini unguja.

## **2.7 Hitimisho**

Dhana ya kazi tangulizi na faida yake, maana ya lugha ikiwa ndio msingi mkuu wa mawasiliano ya wanajami pamoja na kuelezea tawi la isimu jamii ambalo ndilo linaloshughulika na lugha na jamii yaani matumizi ya lugha katika jamii. Mfano wa kazi tangulizi zilizotumika katika utafiti huu, zimesaidiakuelezea tafiti za rejista za maeneo mbali mbali duniani. Pia sura hii imelezea kiunzi cha nadharia kwa kuelezea Nadharia ya maafikiano na ile ya vitendo usemi katika kufanikisha utafiti huu na kumalizia na hitimisho la sura nzima.



## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Mbinu za utafiti zimefafanuliwa na wanaisimu mbali mbali mfano, Kothari (2004) anayesema Mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Pia Kombo na Tromp (2011), wanasema, mbinu za utafiti ni muundo au mpangilio wa kidhanifu ambao huongoza utafiti katika mpangilio au utaratibu wa kukusanya na kuchanganua taarifa (data) katika hali ambayo inalenga kufikia malengo ya utafiti. Hii ina maana kwamba kimuundo, sura hii itafafanua kwa uwazi zaidi eneo ambalo utafiti huu utafanyika, Aidha sehemu hii itazungumzia kwa ufasaha aina ya utafiti ambayo mtafiti alitumia katika utafiti wake, Sampuli na usampulishaji, pia imeelezea njia zilizotumika katika kukusanya na kuchanganua data na kumalizia na hitimisho la sura nzima.

#### **3.2 Aina ya Utafiti**

Utafiti ni wa maskanini (uwandani) hii ina maana kwamba, data au taarifa zinazohusu mada husika zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa walioko maskanini kwa njia mbali mbali mfano, mahojiano, mjadala, ushuhudiaji pamoja na ushiriki wa moja kwa moja Njia nyingi zilimfanya mtafiti kwenda kwenye kundi lengwa na kukusanya data kutokana na maswali yaliyotayarishwa na mtafiti ambayo yanayoendana na mada husika. Mtafiti alichagua aina hii ya utafiti kwa sababu ya urahisi wa kukusanya data hasa kutokana na urahisi wa kulifika eneo husika pia ukaribu wa kuwaelewa baadhi ya makuli katika eneo hilo pamoja na uchache wa gharama za ufuatiliaji yalimsukuma mtaditi wa utafiti huu kutumia aina ya utafiti wa

maskanini kwa dhamira ile ile ya kukamilisha malengo ya utafiti huu kwa ufanisi zaidi.

### **3.3 Eneo la Utafiti**

Eneo la utafiti maana yake ni sehemu maalumu ambayo mtafiti akiwa na sababu za msingi ameichagua na kuitumia katika kufanya kazi ya utafiti wake na kupata taarifa zinazohusu mada husika aliyoichagua. Mtafiti alitumia eneo la bandari ya Malindi iliyopo kisiwa cha Unguja. Kiutawala, bandari ya Malindi ipo mkoa wa Mjini Magharibi, wilaya ya Unguja Mjini katika shehia ya Malindi. Bandari ya Malindi inaonekana upande wa magharibi wa wilaya ya mjini. Kwa upande wa kusini imepakana na majumba ya kihistoria mfano Betl-l-ajabu (nyumba iliyokuwa ya kifalme wa kiarabu) pamoja na majumba mengine makubwa ya kizamani ambayo hivi sasa yamefanyiwa ukarabati na kuwa mahoteli ya kitalii. Na upande wa kusini mashariki imepakana na kituo cha polisi Malindi, kaskazini imechukuana na bahari ya Hindi iliyoingia ndani hadi eneo la Mpigaduri. Watu wa eneo hili shughuli yao kuu ya kiuchumi ni uvuvi, biashara ya kutembeza wageni, biasara ya vinyago na bidhaa za matunda pamoja na uingizaji na ubebaji wa mizigo bandarini. Mtafiti amechagua eneo la bahari ya Unguja iliyopo Malindi mjini Unguja kwa sababu eneo hilo linaenda sambamba na mada ya mtafiti yaani *“Tofauti ya kimaana kati ya rejista inaozungumzwa na wafanyakazi wa bandarini na Kiswahili Sanifu*. Aidha ni pahala ambapo vyombo mbali mbali mfano meli na boti za abiria na mizigo hufunga gati na kazi ya kuteremsha abiria na kupakuwa mizigo hufanywa na wafanyakazi wa bandarini hasa makuli.pamoja na usafirishaji wa abiria. Pia kutokana na urahisi wa wa kufika eneo hilo na urahisi wa utumiaji wa bandari hiyo

na kupata taarifa zinazohitajika ilimsukuma mtafiti kutumia eneo hilo na pia ilisaidia kupunguza gharama za ufuatiliaji. Ramani na picha za eneo la utafiti linaonekana bayana katika viambatanisho hapo chini ambapo makuli wanafanya kazi ya uchukuzi wa kubeba na kupakuwa mizigo huku wakitumia rejista yao ya kundi maalumu ya bandarini.

**Picha no.3,** Picha hii inaonyesha Eneo la utafiti ( bandarini ) Unguja ambako rejista ya makuli hutumika katika kufanikisha kazi ya ukuli hapo bandarini.



### **3.4 Walengwa wa Utafiti**

Utafiti huu ulihusu rejista ya makuli wa bandari ya malindi iliopo mjini unguja ambao wana mtindo wao maalumu wa mawasiliano. Hiki ni kikundi kizima cha makuli wa bandarini ambao wanafanya kazi ya ubebaji wa mizigo hapo bandarini unguja. Makuli hao walikuwa mia moja na thamanini lakini kutoka na taratibu za

kazi hatukuweza kuwafanyia utafiti makuli wote isipokuwa tumewatumia baadhi tu kama ni sampuli ya makuli wote.

**Picha no: 4** inaonyesha baadhi ya walengwa wa utafiti ambao ni makuli wakiwa katika harakati za kubeba mizigo kutoka katika boti la abiria linaotokea Dar- es- salama mara lilipowasili katika bandari ya malindi iliopo mjini unguja.



### **3.5 Sampuli na Usampulishaji**

Katika sehemu hii tumeelezea sampuli na usampulishaji kama ifuatavyo:

#### **3.5.1 Sampuli**

Sampuli ni aina ya watafitiwa (walengwa) ambao wameteuliwa kutoka katika kundi kubwa ili watumiwe katika utafiti. Naye Kothari (2004 ) na Enon (1998 ) wanatoa ufafanuzi kuwa watafitiwa hao wanaweza kuwa watu au vitu ambavyo mtafiti huteua

kwa ajili ya kufanyia utafiti kwa kuzingatia malengo na aina ya utafiti wake. Naye Sorencen (2010) anasema sampuli ni sehemu ya watu kidogo ambayo huwakilisha watu wengi. Babbie (1992), anafasili sampuli kwa kusema ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Sampuli hupatikana kutokana na mbinu anuai za usampulishaji. Kutokana na maana hizo zilizotolewa na wataalamu, tunaweza kuhitimisha maana ya sampuli kwa kusema, sampuli ni wawakilishi wa kundi fulani kubwa ambao mtafiti amewateua ili awatumie katika utafiti wake kwa madhumuni ya kupata taarifa muhimu zitakazohusu aina ya utafiti husika. Hivyo utafiti huu ulihusisha sampuli ya watu wa kundi moja tu la makuli ambalo ndio walengwa wangu yaani wanaobeba na kupakuwa mizigo melini/botini na majahazini na kupeleka sehemu husika. Ulinganifu ulihusisha zaidi kwa maneno ( rejista ) wakati wakiwa kazini na wakiwa nje ya kazi yaani mitaani hasa kwa kuzingatia makuli wengi wameathirika na lugha ya kiswahili sanifu na wanarubia rejista hiyo wakiwa bandarini tu na wakiwa nyumbani waliungana na wanajamii wengine kutumia lugha ya mitaani . Hivyo bado makuli wanaelewa lugha sanifu ya kiswahili ingawa wakifika eneo la bandarini hutumia rejista ya bandarini ambayo ndiyo lugha yao rasmin katika mazingira ya kazi.

### **3.5.2 Sampuli Kielelezo**

Kombo na Tromp (2011) anasema, katika mbinu hii mtafiti hulenga kundi fulani la watu, vitu au dhana zinazoaminika kuwa na uhakika juu ya utafiti husika Kama mtafiti alivyotaja idadi ya makuli katika bandari ya Zanzibar ilikuwa mia moja na thamanini. Ilikuwa ni vigumu kuweza kuwapata wote kwa ajili ya utafiti huu. Kwa

hivyo, tulitumia kikundi kidogo kutoka idadi ya kundi kubwa ili kutuwezesha kufikia lengo letu kwa urahisi. Kulingana na Mugenda Mugenda (2003) anasema hiki kikundi kidogo ni sharti kiwe asilimia 30 ya kikundi kizima. Makuli wa bandarini jumla yao ni mia moja na thamanini lakini mtafiti aliwatumia wachache kama ni kielelezo cha kundi kubwa kama inavyoonekana katika jeduweli hapo chini kupata kikundi kidogo katika utafiti ilikuwa ni makuli hamsini na nne kama inavyojitokeza katika jedwali hapo chini. Kwa kuwa muda aliotumia mtafiti kuwarekodi, kuwahoji pamoja na kwenda kushuhudia maongezi yao hapo bandarini ulitegemea wakati maalumu na mara nyingi siku za kazi ambako harakati ziliendelea hatukuweza kutumia zaidi ya ule wa mazungumzo yao ambao ni nyakati za mapumziko au wakati wa kupata chakula ambao wahusika wengi huwa rahisi kuwapata kwa maongezi. Aidha, katika makundi yaliyofanyiwa mahojiano, mtafiti aliwagawa watu kwa kuzingatia umri wa kuzaliwa tu kwani kazi hii kwa bandari ya unguja inafanywa na jinsia moja tu ya kiume. Watafitiwa wote wotikuwa hamsini na nne, vijana walikuwa ishirini, kundi la makuli watu wazima walikuwa ishirini na mbili, na kundi la viongozi wa makuli (machepe) walikuwa kumi kama inavyoonekana katika jeduweli hapo chini.

**Jedwali 1:** Inaonyesha mgawanyo wa idadi ya makuli hamsini na nne waliofanyiwa utafiti. kama ni Sampuli ya Watafitiwa wakiwa ni miongoni mwa kundi lengwa.

| NO: | WALENGWA            | KE | ME        | JUMLA     |
|-----|---------------------|----|-----------|-----------|
| 1.  | MAKULI VIJANA       | -  | 24        | 24        |
| 2.  | MAKULI WATU WA ZIMA | -  | 20        | 20        |
| 3.  | VIONGOZI WA MAKULI  | -  | 10        | 10        |
|     | <b>JUMLA</b>        | -  | <b>54</b> | <b>54</b> |

**Jedwali 2** Walengwa kulingana na Umri wao.

| MIAK.18-35 | MIAK.36 -49 | MIAK.50 ---- | JUMLA     |
|------------|-------------|--------------|-----------|
| <b>24</b>  | <b>20</b>   | <b>10</b>    | <b>54</b> |

### 3.5.3 Usampulishaji

Kothari (1990) na Suwed (2013), akimnukuu Bryman (2004) wanasema, Usampulishaji ni mchakato wa kufanya uteuzi wa wawakilishi kutoka ndani ya kundi la watu wengi na kuwa wao ndio kigezo na msingi wa upatikanaji wa taarifa muhimu zinazohitajika na mtafiti. Singh (2007) anasema, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Pia wataalamu wengine wanafasili kwa kusema, Usampulishaji ni hatua ya uteuzi wa sehemu ,mfano watu, taasisi fulani, kutoka ndani ya kundi kubwa la watu kwa madhumuni ya kusoma kulingana na malengo ya mtafiti.([www.social/researchmethod.net/w/sampling.php](http://www.social/researchmethod.net/w/sampling.php)) .W.W.W.dictionary.com/browses, Rose Mwaipopo Ako, Mvungi na Anku J. Sanga (1999 ) Usampulishaji ni

hatua ya kuchukuwa idadi fulani ya wawakilishi na kufanya uchunguzi juu ya jambo fulani kutoka ndani ya kundi kubwa la walengwa wa utafiti. .Kutokana na maana za wataalamu hao, mtafiti anahitimisha kwa kusema usampulishaji ni kanuni au hatua ya kuchagua au kuteua sampuli kwa ajili ya kufanya majaribio au uchambuzi juu ya jambo fulani ambalo mtafiti anataka kulifanyia kazi.. Hivyo katika utafiti huu haikuwa rahisi kuwahusisha watu wote wanaotumia bandari ya Malindi Unguja. Mtafiti alitumia mbinu ya sampuli lengwa kama ilivyofasiliwa na wataalamu mbali mbali mfano, Cooper (1989) na Vans (1990) wanafasili kwamba kundi lengwa kuwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti. Hivyo, katika utafiti huu kundi lengwa ni makuli wa Bandari ya Malindi iliyopo mjini Unguja. Katika utafiti huu njia hii imetumika kwa sababu imemsaidia mtafiti kuchagua wahojiwa kutokana na urahisi wa kufikiwa, uchache wa gharama pamoja na ukaribu mkubwa alionao mtafiti na baadhi ya makuli wa bandari hiyo. Mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kupata sampuli ya watu wenye uzoefu na kufahamu misamiati ya makundi lengwa yaliyotajwa hapo mwanzo yenye maskani ya bandari ya Malindi mjini Unguja na hatimaye kupata data ambazo zilikuwa ni kiini cha utafiti huu na kumsaidia mtafiti kufanya majumuisho mahsusi kulingana na malengo ya utafiti.

#### **3.5.4 Usampulishaji Welekeo**

Ni kielelezo cha usampulishaji ambacho kinatoa fursa au nafasi kwa kila mtu, kitu, au eneo linalohusishwa katika uchunguzi. Wahusika wote watakuwa na nafasi na haki sawa ya kuteuliwa wakati wa kutafuta uwakilishi. Aina hii haina upendeleo kwa



muhusika yeyote kwa sababu nafasi ya kuteuliwa inaweza kumuangukia muhusika yeyote la msingi awe yumo kwenye jamii ya walengwa wa utafiti.

### **3.6 Njia na mbinu mbali mbali zilizotumika katika kukusanya data**

Data za utafiti ni taarifa zilizokusanywa kutoka katika vyanzo mbali mbali ambazo zilichambuliwa na kuchanganuliwa kwa lengo la kuibua matokeo ya utafiti. Data hizo zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali kutegemeana na muundo wa mada inayotafitiwa. Kothari (1990) anasema njia au mbinu ya kukusanya data ni zoezi la awali katika kutumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data. Anasema, kila mbinu ya kukusanya data ina ubora na changamoto zake, njia mojawapo ya kupunguza changamoto na kuongeza ubora ni kutumia mbinu zaidi ya moja katika utafiti. Data ni taarifa zinazopatikana baada ya kufanyika uchunguzi juu ya jambo fulan. Kothari (1990) ziko data za aina mbili yaani data za msingi na data za upili. Data za msingi ni zile data ambazo taarifa za moja kwa moja kutoka kwa walengwa zinapatikana. Mfano majarida, tasnifu, vitabu mbali mbali na vitu vyingine. Kwa upande wa data za upili ni aina ya data ambazo zinapatikana kupitia na taarifa zilizohifadhiwa kwa maandishi. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia njia zote yaani ile ya kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa walengwa wa utafiti (Data za msingi) na ile ya kutumia taarifa zilizohifadhiwa kwa maandishi kwa lengo la kupata usahihi na upana zaidi wa data zinazohitajika katika utafiti huu. Best na Kahn (1993) walisisitiza umuhimu wa data za mara ya kwanza ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine yoyote na moja kwa moja zinapatikana kutoka kwa watafitiwa. Katika ukusanyaji wa data mtafiti alitumia vifaa mbali mbali ili aweze

kukusanya taarifa kwa umakini na usahihi mkubwa kama wanavyovipa umuhimu wataalamu wa lugha.

Mulokozi (1983), anaeleza kuwa, vifaa muhimu vya utafiti vilivyopo leo ni kalamu karatasi, tepurekoda, kamera, kamera ya sinema, transleta, kompyuta na transmita. Kombo na Tromp (2006), wanaeleza kuwa, ukusanyaji wa data unahusu kukusanya taarifa mahsusi zilizokusudiwa kutoa au kupinga uhalisia wa mambo fulani. Kutokana na hoja hii ya Mulokozi, mtafiti wa kazi hii alitumia shajara, kamera na kinasa sauti, na kompyuta ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

### **3.6.1 Kompyuta**

Zana hii ilitumika kwa kila hatua kama vile maandalizi kwa kuandika pendekezo la utafiti, ukusanyaji wa data kwa kutunzia kumbukumbu za data zilizokusanywa na uchambuzi wa data katika kurahisisha mchakato wa kuchambua data na mwisho kuandikia tasnifu ya utafiti huu.

### **3.6.2 Shajara**

Hiki ni kitabu cha kuandikia kumbukumbu za matukio ya kila siku. Shajara ilimsaidia mtafiti kutunza kumbukumbu za yale yanayojiri kila siku katika kipindi cha ukusanyaji wa data, ikiwemo idadi ya watafitiwa aliokutana nao, jinsi, mahala na changamoto alizokumbaana nazo

### **3.6.3 Kamera**

Kinachotumika kwa ajili ya kuchukulia picha mgando, zana hii ilitumika zaidi katika hatua ya kukusanya data. Mtafiti alitumia kamera kwa lengo la kuweka

kumbukumbu za utafiti, kama vile kuweka picha za wahojiwa na hata maeneo muhimu, yaliweza kusaidia ufanisi wa utafiti huu. Kifaa hiki kilitumika katika utafiti huu kwa kunasa picha za wahojiwa mbalimbali wanaotumia rejista ya bandarini hasa makuli.

#### **3.6.4 Kinasa sauti**

Kilitumika kurikodi mazungumzo ya watafitiwa hasa wakati wa mahojiano ili kupata uhakika na ukweli juu ya jambo fulani na kujenga ushahidi wenye ukweli. Lengo la zana hii ni kumsaidia mtafiti kuhifadhi data, hasa kwa ile njia ya mahojiano, njia ambayo inakuwa ngumu kuhifadhi data zake kwa mara moja au kuziandika kwa mara moja tena kwa ufanisi. Hivyo ili kurahisisha hatua hii, mtafiti alitumia kinasa sauti kunasa data za mahojiano ili iwe rahisi kuzipitia wakati wa kuandika ripoti ya utafiti. Kama tunavyoelewa vifaa peke yake bila ya kuwa na mbinu sahihi ya kukusanyia taarifa kazi ya utafiti huu itakuwa haijakamilika vizuri. Hivyo, mtafiti aliunganisha na mbinu mbali mbali katika kukanilisha kazi yake kama vile, mbinu ya hojaji, ushuhudiaji pamoja na mbinu ya mahojiano.

#### **3.7 Mbinu ya Hojaji**

Kwa mujibu wa Kothari (keshatajwa) hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watafitiwa ili wayajibu na baadae kurudushiwa mtafiti yakiwa tayari yemeshajibiwa. Walliman (2006), anaongeza kuwa maswali ya hojaji yako ya aina mbili; aina ya kwanza ni ile inayohusisha maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jibu miongoni mwa majibu kadhaa yaliyopendekezwa. Aina hii ya hojaji ni rahisi kujibu na husaidia kupata majibu mahsusi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni

ile inayohusisha Maswali yasiyo funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuwa huru kueleza wanachokijua juu ya dhana fulani kutegemeana na kile kilichoulizwa. Aina hii hutoa uhuru kwa watafitiwa kueleza mawazo yao kwa kuelewa na uwazi na pia husaidia kupata taarifa nyingi zaidi. Kutokana na kuwa na ubora na changamoto katika mbinu hizi, Mtafiti ametumia aina zote mbili ili zisaidiane katika kutatua au kuziba changamoto ambazo zingejitokeza. Mbinu hii ya hojaji ilimsaidia mtafiti kupata data zilizohusu misamiati ya bandarini inayozungumzwa na makuli na wafanyakazi wengine na zilizoonyesha tofauti za kimaana kati ya maneno yanayozungumzwa na wafanyakazi wa eneo la bandarini hasa wapakuaji na wabebaji mizigo (makuli ) na watumiaji wa lugha ya Kiswahili sanifu ambao wanatumia bandari ya Malindi mjini Unguja.

### **3.7.1 Mbinu ya ushuhudiaji**

Ushuhudiaji ni mbinu ya kukusanya data inayohusiana na kushiriki na nakili mienendo ya watu, vitu na matukio katika utaratibu maalumu. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata taarifa za mwanzo zikiwa na ukweli kuhusiana na namna misamiati inavyojitokeza katika mawasiliano yaliyotokea baina ya makundi husika. Mtafiti aliamua kutumia mbinu hii ili kupata data zinazokubalika na kuaminika na kupunguza changamoto. Pia ilimsaidia kupata data za mwanzo zilizohusu rejista kutoka kwa makuli wapevu na waliobobea katika mazungumzo ya bandarini kwa upande mmoja, na kutoka kwa wazungumzaji wa lugha sanifu ya Kiswahili kwa upande mwingine. Kama anavyosema Walliman (keshatajwa) kuwa data za awali ni data zinazoaminika kwa sababu hupatikana au kurekodiwa moja kwa moja kutoka kwenye tukio. Mbinu hii ya uchunguzi imemsaidia mtafiti kukusanya data

zinazohusu maana ya rejista kama zinavyotumiwa na makundi husika na kupata fulsa ya kubainisha tofauti ya kimaana itakayojitokeza baina ya makundi hayo. Aidha data hizi zilimsaidia mtafiti katika kujibu maswali yake ya utafiti kama alivyoyatanguliza hapo mwazo.

### **3.7.2 Mbinu ya mahojiano /usaili**

Kwa mujibu wa Kothari (2009) usaili ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo njia ya mdomo. Kombo na Tromp (2006), wanafasili mahojiano kwa kusema, mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au ya simu, barua pepe na kadhalika yanayofanyika kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Walliman (keshatajwa) ameyagawa mahojiano katika aina tatu ambazo ni mahojiano ya ana kwa ana, mahojiano ya kikundi na mahojiano ya simu (mtandao). Ingawa mbinu hii inaweza kufanywa kwa njia zote hizo. Kutokana na maana hizo ,mtafiti wa utafiti huu alitumia mbinu hii kwa kuwahoji watafitiwa wake kwa ajili ya kupata data zinazoonyesha maana ya maneno/msamiati kwa mujibu wa mazingira ya makuli na matumizi ya lugha ya kiswahili sanifu kwa njia ya ana kwa ana, Kama alivyosisitiza Kothari (2009), mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti huwauliza maswali watafitiwa na wakati mwingine watafitiwa hupata fursa ya kumuuliza maswali mtafiti. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu mbali mbali , mfano kwanza, ni kwa ajili ya kupata ukweli wa majibu ya watafitiwa hasa ukizingatia majibu yanatoka kwa muhusika mwenyewe,. Pia ni rahisi kwa mtafiti kusadifu sampuli yake kwa urahisi na kwa usahihi zaidi. Hii ni kwa sababu mtafiti alikuwa na uwezo wa kuwahoji wakiwa ana kwa ana na kuwauliza maswali na kunukuu majibu yao papo kwa papo wakati

mahojiano yao yanaendelea. Ubora wa njia hii vile vile yale maswali ambayo yatakosa majibu yaliweza kutafutiwa ufumbuzi wakati huo huo. Aidha ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa upana zaidi, kwasababu muulizaji maswali na waliojibu wote walikuwa na uhuru zaidi wa kuulizana maswali na kupata majibu ni fulsa adhimu na ni adimu kupatikana katika mbinu nyengine ya utafiti mfano dodoso. Mbinu ya mahojiano ilitumika kukusanya data zinazohusu maneno ya vifaa mbali mbali vya matumizi ya vifaa yanayolingana kimaumbo lakini yana maana zinazotofautiana na lugha sanifu ya kiswahili Pia mbinu hii ilichunguza taatira ya rejista zinazopatikana hapo eneo la bandari ya ma;indi iliopomjini unguja na kuona athari zake kwa wasafiri na watu wengine wanaoingia na kutoka bandarini. Hivyo data zilizopatikana kwenye mbinu hii zilifaa sana kujibu swali namba tatu.

### **3.8 Uthabiti wa njia za kukusanya data**

Jambo kubwa na la msingi kabisa lakuzingatia katika kutumia njia mbali mbali za kukusanyia data ni kupatikana kwa uthabiti wa utekelezaji wa njia zenyewe na uthabiti wa data zinazohitajiwa na mtafiti, kama anavyosema Kothari (2004) kuwa uthabiti ni kiwango ambacho mbinu za utafiti zitapima kile kilichotakiwa kupimwa na mbinu hiyo. Naye Sigh (2007) anasisitiza kuwa zana/mbinu zote zilizotayarishwa kwa ajili ya kufanyia utafiti ni lazima zipimwe ili kuona kama zinafaa katika mazingira halisi yaliyokusudiwa. Kwa kuzingatia maoni ya wataalamu hao, mtafiti alizipima njia hizo kwa watu ambao sio walengwa wa utafiti huu lakini wanafanana katika viwango vyao vya elimu au shughuli zao za kila sikukabla ya kukusanya data. Lengo la kuzipima hojaji ni kutaka kujiridhisha iwapo maswali yakowazi na hayaonyeshi hali ya utata hata kidogo na yanaeleweka kwa watafitiwa. Pia kujua

iwapo mtafiti atapata data anazozihitaji kulingana na malengo ya utafiti wake. Hivyo, baada ya kuzipima hojaji, mtafiti alipata fursa ya kufanya maboresho na marekebisho kwa zile sehemu zilizohitajika kufanyiwa hivyo, ili ziweze kugawiwa kwa watafitiwa waliokusudiwa kwa ajili ya kukusanya taarifa za utafiti. Mtafitiwa utafiti huu, hojaji zake alizithibitisha kwa kuwapa wanafunzi wa kidato cha nne, tano na sita wa shule ya sekondari ya Lumumba na baadbi ya walimu washuleyasekondari Vikokotoni.

### **3.9 Hitimisho**

Sehemu hii imejikita zaidi katika kutoa maelezo kuhusu aina ya utafiti ambayo ni maskanini, eneo lilofanyiwa utafiti huo ambalo ni bandari ya Malindi iliopo mjini Unguja, walengwa wa utafiti ambao ni makuli, mabaharia na wafanyakazi wa kawaida wa bandarini pamoja na kufafanua maana ya sampuli na usamplishaji. Aidha sehemu hii imezungumzia uthibiti wa njia za kukusanyia data ambapo watu wasio walemgwa wa utafiti walitafutwa ili kuzithibitisha njia za utafiti zilizotumiwa na kufanya majaribio ya njia mbali mbali za kukusanyia data kama vile hojaji, ushuhudiaji na usaili. Mwisho mtafiti alieleza ni kwa namna gani data zimeweza kuchambuliwa.

## SURA YA NNE

### UCHAKATAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Kabla ya kuzichanganua data, Mtafiti alichakata data alizozikusanya, kwa kuzitenga zile zinazofaa kulingana na aina na malengo ya utafiti na zile zisizofaa kuziweka kando. Uchanganuzi wa data ni muhimu sana katika kazi yoyote ya utafiti kama wanvyosema Jamal na Kamuzora (2008), wakimnukuu Kothari (2004) kwamba uchambuzi wa data ni mchakato wa kuchanganua taarifa fulani zilizopo ili kupata mpangilio wa mahusiano miongoni mwa makundi mbali mbali ya taarifa zilizokusanywa katika utafiti huu. Katika sura hii, data zilizokusanywa zimewasilishwa na kujadiliwa ili kujibu maswali ya utafiti, na hivyo kufikia malengo ya utafiti. Uwasilishaji wa data umegawanywa katika sehemu zifuatazo: kwanza kutoa ufafanuzi juu ya tofauti ya kimaana kati ya maneno yanavyotumi katika lugha sanifu ya Kiswahili na rejista ya bandarini. Pili, sababu zilizosababisha kuibuka kwa rejista ya makuli hapo bandarini, Tatu, taathira zinazojitokeza wakati wa utumiaji wa rejista hiyo hasa kwa wasafiri na watu wengine wanaofika bandarini kwa matembezi. Sura hii pia inaonyesha kiwango cha majibu yaliyotolewa kwa asilimia kutokana na uchanganuzi wa taarifa zilizokusanywa na mtafiti kama inavyoonekana katika jeduweli hapo chini na kumalizia na hitimisho la surah hii.



**Jedwali no. 3. inaonyesha idadi ya makuli na kiwango cha Majibu kilichotolewa  
baada ya uchanganuzi wa taarifa zilizokusanywa.**

| <b>S</b>     | <b>WATAFI-TIWA</b> | <b>ASILIMIA</b> | <b>SABABU ILIYOTOLEWA</b>  |
|--------------|--------------------|-----------------|--|
| 1            | 10                 | 18.51           | Muingiliano wa makuli kutoka jamii tofauti   |
| 2            | 26                 | 48.24           | Aina na ugumu wa Kazi yenyewe yaani ukuli.   |
| 3            | 6                  | 11.11           | Inaonekana makuli wengi wamesoma kidogo au hawakusoma kabisa elimu ya shule. na hivyo,hawana lugha rasmi. Rejista imekuwa ni lugha ya ukombozi wa kiuchumi kwao. |
| 4            | 12                 | 22.22           | Kumejitokeza tathira chanya na hasi .Mfano kuoneana makuli hawana adabu na wanapenda matusi tu jambo ambalo walengwa wa utafiti wanapinga dhana hiyo potofu.     |
| <b>JUMLA</b> | <b>54</b>          | <b>100</b>      |  |

**Chanzo: Data za uwandani**

Baada ya mtafiti kuzichambua data zilizokusanya kupitia vyanzo mbali mbali kama nilivyovitaja hapo mwanzo, mtafiti amegunduwa mambo yafuatayo:

#### **4.2 Tofauti ya kimaana kati ya rejista ya makuli na lugha ya kiswahili sanifu**

Katika kufanya majadala huu mtafiti ameanza na lengo mahsusi la kwanza ambalo ni kubainisha tofauti ya kimaana kati ya rejista ya makuli wa bandarini unguja na lugha ya Kiswahili sanifu. Kama ilivyoelezwa katika 1.3.2, utafiti huu uliongozwa na nadharia tatu lakini ka bahati njema lengo la kwanza limeongozwa na nadharia ya isimujamii ya msimbo ambayo kwa mujibu wa Bernstrei (1964) nadharia hii ina misingi miwili mikuu ambayo ni msimbo finyu na msimbo pana ambazo zinazungumzia upana wa maana ya rejista au ufinyu wa maana hizo na kubaini maana mbalimbali za rejista ya makuli wa bandarini na kugunduwa kwamba hakuna tofauti kubwa kati ya rejista ya makuli wa bandarini unguja na lugha ya Kiswahili sanifu. Utafiti, ulionyesha kwamba hakuna tofauti kubwa za kimaana kati ya rejista ya bandarini namaneno ya lugha ya Kiswahili Sanifu. Kinachotofautisha ni tuni ya utamkaji wa maneno yenyewe tu, kwani wazee wengi wa mitaani wanasikia na pia wanaelewa kuli anataka nini. Kwa mfano kuli anaposema “sumile huko “yaani kaa upande apite” Wazee wengi wanaelewa lakini neno hilo hilo linapotoka mdomoni kwa kuli hasa akiwa katika harakati za kazi huwa lina tuni yake maalumu ambayo kwa wageni huwa ni vigumu kuelewa kwa siku za mwazoni ila mgeni akizoea mazingira ya bandarini huelewa kinachozungumzwa na makuli. Hata hivyo yapo baadhi maneno yenye maana tofauti na lugha sanifu ya Kiswahili mfano rejista ya nipe nyuma (anahitaji njia akiwa na mzigo) ambapo kwa lugha ya Kiswahili sanifu maana yake anahitaji makalio. Pia kuli anpomuamrisha kuli mwezake hasa katika ugavi wa kitu, mmoja husema mpige mkundu wa ndoo huyoo, kwa maana apewe kitu kidogo tu.

Hivyo mtafiti amehitimisha kipengele hiki kwa kusema hakuna tofauti kubwa kati ya rejista ya makuli wa bandarini na maneno ya lugha sanifu ya Kiswahili, zaidi ni kusoma na kuelewa tuni inayotolewa na makuli wenyewe kwa kufika eneo lao la kazi na kuwasikiliza.wanapowasiliana.

Tofauti hizi za kimaana pia zinaonekana katika lugha za kigeni kwa kuzingatia rejista tofauti, mfano:

- (i) Underground - British English
- (ii) Subway - American English

Maneno haya yote Yana maana moja yaani ni barabara zipitazo chini ya ardhi. Naye Simpasa na Lipembe (1999) wanaeleza kuwa wazungumzaji wawili wa lugha moja wanaweza kuwa wanatofautiana katika matamshi, kwa sababu wanatoka katika maeneo yanayotenganishwa na milima, bahari au mito na mara nyingine eneo la kiutawala,

### **4.3 Sababu za Kuibuka Rejista ya Makuli Bandarini Unguja**

Katika kufanya majadala huu mtafiti ameendelea na lengo mahsusi la pili ambalo ni kubainisha sababu za kuibuka rejista ya makuli wa bandarini unguja kama ni kundi moja kuu la kijamii lenye mfumo wa utambulisho katika mawasiliano ya kila siku hasa wakiwa katika mazingira ya kazi hapo bandarini unguja kama ilivyoelezwa katika 1.3.2 ,katika nadharia tatu zilizotumika katika utafiti huu , nadharia ya pili ya maafikiano ya Gilies ilitumika na kuwa ni muongozo mzuri katika kugunduwa sababu hizo na kuzifafanuwa kwa upana zaidi. Nadharia hii misingi yake mikuu ni muingiliano na muktagha na msingi wa pili li ulahaishaji wa mtu binafsi katika

makundi Kwa kuzingatia misingi mikuu ya nadharia ya maafikiano ambayo hutokea kutokana na maingiano ya watu wanaotoka katika jamii tofauti, muongozo wa nadharia hii umesaidia kugundua sababu za kuibuka rejista ya makuli wa bandarini unguja ambayo ni pamoja na aina na ugumu wa kazi ya ukuli, maingiliano ya watu kutoka jamii tofauti kila mmoja akiwa na lugha yake ya asili na huku wakitaka kuwasiliana na kutambuana katika harakati za kazi ya ukuli. Mfano makuli walitoka vijiji kama Mkwajuni, kivunge, potoa eneo la kaskazini la kisiwa cha unguja, chwaka, Dunga, uzini e,bambi eneo la kati pamoja na maeneo mengine ya kisiwa cha unguja Aidha, viwango vidogo vya elimu viliwafanya makuli wawe na maingiliano ya karibu sana kwani wote wajiona ni watu sawa hakuna aliyejiona ni bora kuliko mwezake, hivyo ile hali ya kutokujiona bora ikiwa kwa elimu yake au kipato chake na wote kukubali kuwa jamii moja ya makuli pia ni sababu ya kuibuka kwa rejista ya makuli wa bandarini unguja. Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kwamba kazi ya ukuli mara nyingi inafanywa na watu waliokosa elimu ya darasani na maisha yao kuwa magumu na kukosa kazi ya kufanya ambayo itawapatia kipato hivyo, kazi ya ukuli ilikuwa ni mkombozi wa maisha yao. Ingawa kazi ya ukuli ilionekana ni ngumu, inahitaji ujasiri na uvunilivu mkubwa na kinyume chake haihitaji elimu kubwa au usafi wa hali ya juu pia ni kazi ambayo ujira au kipato chake hutegemea uzima wako ,nguvu,kufika kwako mapema katika eneo la kazi na ubora wa afya ya muhusika. Makuli wachache ndiyo wanaobahatika kuwa na hali nzuri kimaisha na walio wengi hufariki wakiwa maskini sana. Mtafiti anahitimisha katika eneo hili kwa kusema nadharia ya maingiliano ya Gilies imekuwa ni dira nzuri ya kuweza kufikia ufumbuzi wa lengo mahasusi la pili.

#### 4.4 Athiri ya Rejista ya Makuli kwa Wanajamii Wengine

Kama mtafiti alivyoeleza kabla kwamba kutokana na udhaifu wa nadharia moja kukidhi haja ya kujibu maswali yote ya utafiti ,mtafiti pia alitumia nadharia ya vitendo usemi iliyoasisiwa na wana filosofia Austin na Searle (1975) katika kupata jibu la lengo mahasusi la tatu ambalo ni kubainisha athari za rejista ya makuli kwa watumiaji wengine. Nadharia hii inazungumzia mambo mawili yaani kusema na kutenda (usemi na utekelezaji wa tendo) taarifa inayotolewa na kiongozi wa makuli haijadiliwi bali ni kutekelezwa tu pila ya pingamizi yoyote. Hivyo, kwa kupitia nadharia hii athari moja inayojitokeza ni utii na heshima kwa makuli hasa wakiwa kazini kama walivyo maskari kwa wakubwa wao, hii inatokana na utekelezaji wa amri zinazotolewa kihalali.

Vile vile athari nyengine iliyoonekana na mtafiti ni ujenzi wa dhana isio sahihi kwa watu wasikuwa makuli. Kwa mfano kitendo cha kuli kuomba njia akiwa na mzigo na kusema naomba nyuma , watu hao huwatia hofu na kujenga dhana kwamba makuli ni watu wahuni a hawafai katika jamii ya watu wanaoheshimiana wenye utamaduni wa aina moja au unaofafanana jambo ambalo sio sahihi. Hii pia ni athari kubwa kwani imejengeka katika akili za watu wasiokuwa makuli na kuonekana muhusika kuli ni mtu mbaya hata akiwa nje ya mazingira ya kazi ya ukuli. Vile lile jamii ya makuli inapata athari kubwa ya kuumia au kupoteza maisha wakati wa kutekeleza amri au usemi unaotolewa na mkuu wao hasa pale utekelezaji wake unapokuwa wa haraka haraka au wa kushindana. Mfano, baadhi ya makuli wanaangukiwa na gunia wakati wa kupanga na kuumia, kugongwa na magari yanayobeba mizigo hapo bandarini pamoja na kulipwa ujira mdogo usiolingana na kazi husika kwa kuonekana

lazima atafanya kazi kwa sababu hana pa kukimbilia na kupata kipato cha kuesesha maisha yake na familia yake kwa ujumla. Hata hivyo mtafiti amegunduwa kwamba mfumo wao wa maisha ya makuli ni wenyewa wameuridhia na kuukubali hasa ukizingatia muhusika anapata ujira kwa kuvuja jasho lake mwenyewe pasipo na hata chembe yoyote ya rushwa. Na mapato yanayopatikana ni halali kufanyia jambo lolote kama kutoa sadaka kwa wanyonge au kwenda kuhiji Makka kwa wale waislamu. Hivyo, kazi ya ukuli ni kazi halali kama zilivyo kazi nyingine na wenyewe wanaipenda na kuithamini sana na mtu yoyote anakaribishwa kufika bandarini na kujiunga na umoja huo baada ya kukubali kufuata masharti na miongozo yao mmoja wapo ni kuwa mvumilivu sana kwa yote yatakayokutokea wakati wa kazi hasa kwa yale ambayo hayana madhara kwa muhusika kuli.

#### **4.4.1 Mahusiano ya Lugha na kundi Lengwa la Jamii ya Makuli**

Baadaya ya kutoa ufafanuzi juu ya malengo mahasusi mtafiti alichunguza uhusiano uliopo baina ya lugha ya kiswahili sanifu na mawasiliano ya kundi lengwa la watafitiwa na kugunduwa kwamba Lugha ya makuli wabandarini iliweza kubainishwa kwa namna ilivyokuwa inatumiwa katika kuwatambulisha. Wachukuzi wa bandarini ndio kiungo muhimu katika kubeba na kuteremsha mizigo bandarini. Kutokana na uhalisi wa kazi yao, wao huhusiana na watu wa matabaka mbalimbali na walio na vyeo tofauti tofauti katika nyanja mbalimbali. Wao hutumia lugha kwa namna inayowatambulisha wao kama kikundi maalumu ambacho kinaweza kutambuliwa kutokana na rejista yao. Kama wasemavyo Linda na Wareing (1999:143), kikundi fulani hutambuliwa kama kikundi cha kijamii na watu wengine kutokana na upekee wa matumizi yao ya lugha na tabia katika eneo lao la kazi.

Matumizi sahihi ya lugha huambatana na makundi ya kijamii kuibua mitindo na istilahi zao zinazowawezesha kurejelea shughuli za kundi husika. Hii inaashiria kuwa kila kikundi katika Nyanja mbalimbali huwa na mtindo wake wa kutumia lugha kwa namna ambavyo itawawezesha kuafikia malengo yao ya kazi. Makuli wa bandarini kama kikundi cha kijamii pia huwa na mitindo na istilahi zao ambazo huwawezesha kutekeleza majukumu yao. Kwa mujibu wa Fishman (1972) jamii ni ya muhimu kuliko lugha na kwa hivyo anasema kuwa jamii ndiyo hutuwezesha kupata muktadha ambao unaweza kutusaidia katika kutazama aina ya lugha inayotumiwa. Kama asemavyo Bernstein (1964), tofauti za kiisimu za matumizi ya lugha ya kikundi fulani hutokea katika mazingira halisi ya kijamii na vyeo vya makundi mbalimbali huweza kubainishwa na usemi wao. Ni rahisi kuchunguza rejista ya makuli wa bandarini wanapokuwa katika eneo la bandarini kwa kuwa hayo ndiyo mazingira yanayowatambulisha na ndio muktadha wao halisi. Fishman (1972) akimnukuu Halliday anasema uchunguzi wa muktadha wa mazungumzo hutuelekeza katika uchanganuzi wa hali na matumizi ya lugha.

Pride (1971:25) anasema kuwa mawanda ya matumizi ya lugha huelezwa kama hali ambapo matumizi ya aina fulani ya lugha hutumiwa na kikundi mahsusi na hii husaidia katika utambulisho wa kikundi hicho cha kiisimu na kwa njia ya kijamii. Hii inaashiria kwamba kikundi fulani cha watu huweza kuainishwa kijamii na kiisimu. Naye Hirst (1986) anasema kuwa namna watu hutumia lugha husababishwa na mambo mawili: wao kama watu binafsi au wao kama wanajamii. Hii ina maana kuwa, lugha wanayotumia katika mazungumzo huchangia katika kujitambua na pia lugha yao ni chombo cha kudhihirisha kikundi hicho husika. Kutokana na maelezo

ya wataalamu hawa, ni wazi kuwa kila kikundi katika nyanja mbalimbali huwa na namna yao ya kuwasiliana. Hii huwatambulisha watu wa kikundi hicho. Muundo wa kitabaka huathiri elimu na kazi za watu na kisha kuwapa wanajamii husika mahusiano fulani ambayo hutambulisha tabaka lao ambalo huwa tofauti na matabaka mengine. Wanajamii katika kikundi fulani hutumia lugha kwa njia ya kipekee wanapoingiliana ili kutambuliwa katika kikundi hicho.

Hii inadhihirisha kwamba unaweza kuzungumza kama wanakikundi hicho na hivyo kuwa mwanakikundi. Hapa Unguja Kwa mfano, kutokana na utafiti huu tumegunduwa kwamba; lugha ya makuli kuchanganya ndimi, sauti yao hudhihirisha mamlaka na wana misimbo yao ambayo hutumiwa katika mawasiliano miongoni mwa. Msimbo ukiwa ni sehemu ya lugha na ni utaratibu wa kutoa mawasiliano ambapo hujitokeza katika hali ya ufinychanya, (Iribemwangi na Mukhwana, 2011:45). Wanaendelea kusema kwamba kwenye msimbo finyu, wazungumzaji huweza kutumia ujuzi na tajriba zao za pamoja na uelewa wa pamoja kusemea kile wanachotaka kuongea au kusema. Aina hii ya msimbo huunda upamoja ambao hufanya watu wanaotumia lugha kuhisi kuwa wao ni wa kundi fulani. Kama mkakati wa mawasiliano, baadhi ya watu hasa maafisa wa usalama hutumia msimbo finyu kama njia ya kuonyesha umoja na kutenga makundi mengine hasa wanapozungumzia masuala yanayohusu usalama wa nchi. Pia hutumia msimbo pana wanapowasiliana na wateja wao. Back to Swahili Hub: Upekee wa sifa ya makundi ya jamii katika matumizi ya lugha.

Mekacha (1993) anasema jamii imeundwa na jumla ya mtu mmoja, kila mmojakatika upekee wake na ndiyo chimbuko la kila kitu ikiwa ni pamoja na mabadiliko katika



jamii na uhusiano kati ya lugha na jamii.” Jamii ni watu, kila mmoja akiwa na upekee wake ila wanapoungana na kuwa pamoja kwa sababu fulani, basi wanakuwa na tabia fulani zilizo sawa katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingati mipaka baina yao Linda na Wareing (1999:143) wanasema kuwa utambulisho wa kijamii si jambo ambalo mtu binafsi anaweza kujiamulia mwenyewe; inategemea na namna watu wengine wanavyowachukulia. Hii ina maana kwamba ni vigumu kwa mtu binafsi kujitambua mwenyewe katika kikundi fulani. Watu wengine walio nje ya kikundi hicho cha kijamii ndio hukutambulisha na kikundi hicho kutokana na kuwa na tabia fulani zilizo sawa na washiriki wengine wa kundi hilo. Wanaendelea kusema kuwa mtu binafsi anaweza tu kutambua hadhi yake katika kikundi kutegemea na cheo alichonacho. Kazi ya makuli inakuwa pia na wakubwa wao ambao wanaitwa “**Machepe**” walio katika vyeo mbalimbali akiwemo chepe mkuu na wasaidizi wake ambao kwa mujibu wa taratibu zao wao hufika bandarini lakini hawabebi mizigo kazi yao kubwa ni kugawa kazi tu na kuisimamia iende vizuri. Hawa ndio hujitambua kwa cheo chao. Panapotokea mgawanyo wa kazi au mapato wao huwa msitari wa mbele kuzigawa kulingana na vyeo vyao pasipo kuangalia ugumu au wepesi wa kazi na akitokea mmoja kulalamika kwa jambo lolote atasimamisha kazi na wale machepe na zile rejista za matusi ya nyuma nini zitamshambulia kwa wingi. Kwa mfano ataambiwa “**je unafikiri nyonyo la bibi lile “ fanya kazi we”**”. Hii inaonyesha kuwa utajitambua tu na kikundi hicho kutokana na cheo chako lakini kama huna cheo, basi wewe ni kama washiriki wengine wa kikundi hicho ambao hutambuliwa kuwa katika kikundi fulani na watu wengine. Kuna mambo mengi ambayo hutambulisha watu wa kikundi fulani cha kijamii; wanaisimu hawa wametaja baadhi yao kama vile mavazi au vitendea kazi lakini pia baadhi ya mambo

fulani ya kiisimu huweza kutumiwa kutambulisha kikundi cha kijamii. Makuli wa bandarini wana tabia zinazowatambulisha kama jamii moja. Hii inatokana na mazoea waliyonayo yaka zi. Fishman (1972) akimnukuu Homans, anasema kadri watu wanavyoingiliana, ndivyo wanazidi kufanana katika hali fulani katika shughuli zao na mazungumzo yao huwiana. Makuli wa bandarini huingiliana wanapokuwa katika mazingira ya kazi. Mazoea haya yamewafanya kuwasiliana kwa njia ambayo inaweza kutumiwa kuwatambulisha wao kama jamii. Hii imewafanya makuli binafsi kupunguza mipaka baina yao na kujikuta wakizungumza kwa namna moja. Kutokana na hali hiyo tunaweza kuhitimisha kwa kusema, jamii ni kikundi cha watu wa sifa fulani mahsusi ambazo zinaweza kutumiwa kuwatambulisha. Hali ya upekee wao wa kutenda au kuzungumza ni baadhi ya mambo ambayo huwafanya kuitwa jamii moja.

#### **4.5 Hitimisho**

**K**atika matokeo haya mtafiti alihitimisha kwa kusema kwamba, Rejista ya makuli ni aina ya lugha maalumu inayotumiwa na kundi maalumu la kijamii katika pahala maalumu mfano bandarini na haiwezi kutumika sehemu nyingine yoyote ambayo hakuna harakati za ubebaji na upakuaji wa mizigo au bidhaa. Mazingira ya rejista ya makuli yanafanana sanana mazingira ya rejista nyingine kama rejista ya msibani, harusini, shuleni, sehemu za ibada na hata hotelini ambako wanajamii walio katika kundi moja na kufanya shughuli zao kwa pamoja wanatumia rejista hizo. Hivyo, kutokana na dhima ya rejista ya makuli wa bandarini ambayo ni kuhimiza na kuchangamsha kazi zao ili zifanyike kwa ufanisi mkubwa. Aidha ni moja kati ya chachu muhimu inayoongeza msamiati wa lugha na kufanya lugha ya Kiswahili kuwa tajiri wa maneno na kujitosheleza katika mawasiliano.

## SURA YA TANO

### MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Rejista ya makuli wa bandarini Unguja imedhihirisha uwepo wa matumizi ya msimbo pana na msimbo finyu. Msimbo pana hutumika wanapozungumzia mambo ya kawaida ya maisha ya kila siku kama vile shughuli za kilimo uvuvi, na mazingira kwa ujumla. Makuli hutumia msimbo pana ili kuwasilisha hisia zao. Mazungumzo haya hueleweka na kila mshiriki wa mazungumzo hayo. Matumizi ya msimbo pana na msimbo finyu yamedhihirisha kuwa nadharia ya misimbo ya Bernstein inagusa rejista ya makuli wa bandarini Unguja. Lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo ya makuli huku wakichopeka maneno ya masihara au lugha zao za kijijini. Mazungumzo ya wachukuzi wa bandarini husheheni kukatizana semi. Kukatizana usemi husaidia katika kuhakikisha kuwa kila mshiriki aliye na jambo amelisema bila kusubiri wenzake wamalize kuongea. Kuchanganya ndimi na kukatizana semi kunaonyesha kuwa pana maafikiano baina ya makuli au wachukuzi wa bandarini. Maafikiano haya yanawatambulisha makuli kama kikundi maalum cha kijamii. Mazungumzo baina ya makuli na matajiri wao ambao ni wafanya biashara na wasafiri mbali mbali wanaotumia njia ya usafiri wanaopitia bandarini Unguja yamedhihirisha kuwa makuli wa bandarini wana mamlaka na pia wana muundo wa uongozi mfano wana chepe na msaidizi chepe au sarahangi. Mazungumzo ya makuli kulingana na mamlaka yao kwa matajiri wao hulazimika kutenda kitendo fulani baada ya usemi wa makuli hao, hali hii huashiria kuwepo kwa athari fulani. Mbinu yetu ya utafiti ilikuwa ni kurekodi mazungumzo ya makuli, kushuhudia maongezi yao kwa kufika eneo la kazi pamoja na kuwahoji wahusika wa eneo hilo ambao ni

wachukuzi wa mizigo wa bandarini ambao ni makuli. Hii ilimwezesha mtafiti kupata data alizohitaji katika uhalisia wake. Nadharia ya vitendo usemi imeakisi sana rejista ya wachukuzi au makuli wa bandarini Unguja.

## **5.2 Mapendekezo kwa wasomi na watafiti wajao.**

Isimu ikiwa ni sayansi ya lugha ina uwanja mpana wa kufanyia utafiti katika kipengele cha lugha, mtafiti hawezi kuchunguza mambo yote kwa wakati mmoja, katika utafiti huu nilikumbana na changamoto kadhaa. Hata hivyo, sikuweza kuzichunguza kwa pamoja hii ilitokana na kubanwa kwa upeo na mipaka yetu kwani kuna mambo mengi ya kutafitiwakatika eneo hili la Bandarini ambapo nililazimika kuyaacha nje. Kutokana na matokea ya utafiti huu tuligundua kuwa rejista ya makuli ya bandarini Unguja na makuli wa bandari ya Bara wanatofautiana kwa baadhi ya maneno mfano upande mmoja wanaita rikwama wengine mkokoteni hivyo, tunapendekeza watafitiwajao wachunguze tofauti ya utamkaji baina ya rejista za makuli wa bandari ya Unguja na makuli wa bandari ya Dar-alama pia wachunguze nafasi ya lugha asilia za makuli wenyewe katikamaongezi wanapokuwa katika eneo la kazi. Hii itawezesha kupata mawanda mapana ya matumizi ya lugha katika maeneo maalumu ya kazi za kijamii Kama bandarini. Vile vile tafiti huu haukuonyesha tofauti ya rejista ya makuli walio na viwango tofauti vya elimu. Hivyo, tafiti zifanywe kubainisha iwapo makuli wenye elimu wanatumia rejista ya aina moja nawale wasio na elimu au hapana. Vile vile utafiti huu ulijikita katika mazungumzo ya makuli bila kuzingatia nafasi ya lugha za vijana katika eneo la bandarini hasa ukizingatia vijana wengi hawana ajira na wanafika bandarini kutafuta kazi, hivyo Mtafiti anapendekeza watafiti na wasomi wajao wafanye utafiti ili

kubaini athari ya matumizi ya lugha za vijana kwa uhai na maendeleo ya rejista ya makuli wa bandarini Unguja hasa ukizingatia vijana wana rejista zao na pia wananguvu tofauti na wazee na vile vile wana matarajio tofauti katika maisha yao ya kila siku.

### **5.3 Hitimisho**

Katika kuhitimisha kazi yetu tunasema kwamba, Matokeo yameonyesha kuwa makuli wa bandarini huchanganya ndimi, hutumia msimbo pana na msimbo finyu na pia hudhihirisha mamlaka yao wanapozungumza na matajiri wao. Hivyo kulingana na maudhui ya nadharia tete kuna ukweli ndani yake. Aidha nadharia tete imedai kuwa rejista ya wachukuzi au makuli wa bandarini ina uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu yao. Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kuwa makuli wa bandarini wanapozungumza na matajiri wao hudhihirisha mamlaka na pia huwataka wenye mizigo kushirikiana nao ili kurahisisha kazi hasa wanapopatana bei ya mzigo kama nadharia tete ya tatu inavyodhihirisha ukweli huo, Matumizi haya ya mamlaka ya hufanya kazi ya ubebaji wa mizigo kuwa rahisi zaidi. Vile vile athari za usemi wa makuli wa bandarini hupelekea kutokea kwa vitendo ambavyo kiisimu tumeviita vitendo usemi. Hivyo, vitendo hivyo vinaonyesha kuwepo kwa kundi maalumu la kijamii na hivyo kuwa na rejista yao ambayo ni sehemu ya mawasiliano katika kazi zao hapo bandarini.

### MAREJELEO

- Adams, J. na Kamuzora F. (2007). *Research Methods for Graduate Bussiness and Social*. Dar es Salaam: DUP.
- Babbie, E. (1992). *The basic Practice of social Research*: London: Wadsworth Publishing Company.
- Batibo, H. M. (1982). “Mawazo ya Mwanzo kuhusu Uhusiano wa Lahaja za Kiswahili za Kusini.” Makala katika Kongamano la Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Benstrin, B. (1964). “Elaborated and Restricted code: Their social Origin and Stone Consequence.” *Journal of Languge Studies Vol. 4*.
- Bright, W. (1992). "Narrow Bantu 'S'" in *International Encyclopedia of Linguistics, Vol.4*.
- Brown, G. (1979). *Speaker listiners and communication Explaration in Discourse Analysis*. New York: Cambridge Press.
- Campbell, L (2004), *Historical Linguistic; An Introduction* (chapter two), Cambridge: Cambridge University Press.
- Enon, J. K (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University.
- Fishman, J. A. (1972). *Language in Sociocultural Change*. (Dil. Annwa S. Ed) California Stanford Univesity Press.

- Grimes, Habwe J. na Wezake (2010). *Darubini ya Isimu Jamii kwa Shule na Vyuho*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Holliday, M. A. K. (1978). *Language as Social semiotic: The social Interpretation of Language and Meaning*: New York: New Age International.
- Holliday, M.A. K. (1985). *The Study of Language* (2<sup>nd</sup> edition ). Cambridge: CUP.
- Hudson, R. A. (1993). *Sociolinguistics*. London: Cambridge University Press.
- Kombo na Trump, D. L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Panline Puplication Africa.
- Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.
- Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology: Method and Technique*. New Age International (P) Ltd.
- Kothari, R. (2004). *Research Methodology: Method and Technique*. New Age International (P) Ltd.
- Massamba, D. B. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mathoko, P. M. (2007). *Isimu jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Kenyatta University.

- Mekacha, R. D. K. (1993). *The Sociolinguistic Impact of Kiswahili on Ethnic Community*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mgullu, R. S. (1990). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Nairobi Foundation Ltd.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Nairobi Foundation Ltd.
- Mulokozi, M. M. (1983). "Utafiti katika Fasihi Simulizi." Katika makala ya Semina ya Kimastaifa ya Waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.
- Nkwera, F. (1989). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Oxford Advanced Learners Dictionary of current English (2000). Oxford: Oxford University Press.
- Schiffrin, D. (1994). *Approaches to Discourse*. Oxford: Bkav Publishers.
- Sengo, T. S. Y. (2009). *Tungizi ya Muyangatwa*: Dar salaam: AERA.
- Sigh, K. (2007). *Qualitative Sociol research Methods*. New Delhi. SAGE Publications.
- Simpassa, H. & Lipembe, P. P. (1999). *Engliah Language II*, Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.



- Trugill, P. (2000). *Sociolinguistics. An Introduction to Language and Society*. London: Penguin Books.
- TUKI, (1990). *Kamusi ya lsimu na lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributers.
- Wamitila K .W. (2004). *Kichecheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Focus Puplication Ltd.
- Whitely, W. H. (1969). *Swahili the Rise of a National Language*. London: Sage Publications Ltd.
- Williman, N. (2006). *Social Research Method*. London: Sage Puplications Ltd.
- Williman, N. (2011). *Research Project- A step- by step- Guide for the First Time*. London: Sage Publication.
- Yule, A. (1993). *The Study of Language*. London: Cambridge University Press.

## VIAMBATANISHO

### Kiambatanisho1: Hojaji la Utafiti

Jina la mtafitiwa ..... (siyo lazima kuliandika)

Umri/ (miaka)..... jinsi-m:ke (.....) mume (.....)

#### Kiwango cha Elimu.

Diploma ( ), Fvi ( ) Fiv( ), kidato cha ii (.....) Std vii ( ) sikusoma (.....)

Weka alama ya vyema panapostahiki,

Eneo la makazi: Shehia unayoishi .....

Mtaa/kijiji.....

Kitongoji .....,

Weka alama ya vyema idadi ya miaka uliyofanya kazi ya ukuli katika bandari ya

Unguja.

0 - 5 ( ), 5 - 10 ( ), 10 - 15 ( ), 15 - 20 ( ), 20 na kuendelea ( )

Andika maneno 10 mnayotumia wakati wa kazi za ubebaji wa mizigo hapa bandarini ambayo huwezi kuyatumia mukiwa katika mazingira mengine mfano nyumbani.

Msibani vilabuni, mpirani, msikitini, kanisani n.k

1. ....
2. ....
3. ....
4. ....
5. ....
6. ....
7. ....

**Kiambatanisho cha 2:** Jaduweli linalofuata linaonyesha Baandi ya ya maneno ambayo mtafiti aliyagundua katika utafiti wake ambayo yalitumika kuwa ni rejista ya makuli wa bandarini Unguja na maana zake zilizolinganishwa na maana halisi katika lugha ya Kiswahili sanifu.

| <b>REJISTA YA MAKULI</b> | <b>MAANA KATIKA MAZINGIRA YA BANDARINI</b>  | <b>MAANAKATIKA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU</b>                                   |
|--------------------------|---|--|
| Abadari                  | Kaa vizuri nipite   | Kuwa na tahadhari  |
| Sumile                   | Kaa kando mzigo mzito uko begani  | Nipishe nakuja na kitu kizito.   |
| Nipe myuma               | Tazama mzigo unakuja.   | Nipatie sehemu ya nyuma ya mwili au makalio.                                   |
| Tandoo                   | Njoooni (kuna kazi imewadia).   | Wito maalumu wa makuli   |
| Chepe                    | Mkuu wa kikundi cha makuli (kiongozi).  | Ni mtu anayepeda kufanya masihara mbele ya jamii                               |
| Sekandi chepe            | Msaidizi wa mkuu wa kikundi cha makuli.   | Ni mtu wa pili kwa kupenda kufanya masihara.                                   |
| Kuli                     | Ni mpakuzi na mbebaji mizigo kutoka melini na kuja bandarini au kuingiza melini.              | Ni jina la mtu anayefanya kazi za uchukizi wa mizigo katika eneo la bandarini. |
| Wapagazi                 | Ni watu wanaobeba mizigo kwa kutumia mikokoteni   | Ni aina ya wachukuzi wa mizigo.  |
| Kuchukuza                | kufanya kazi ya kubeba mizigo bandarini au sehemu yoyote kama sokoni anbako mizigo inapekekwa | Ni kazi maalunu ya ubebajiwa mizigo anayoifanya mtufulani.                     |

|                |   |   |
|----------------|---|---|
| Mchukuzi       | Ni mtu anayefanyakazi ya kubeba mizigo bandarini.   | Ni mtu anyebeba mizigo pahala popote  |
| Rasa           | Mzigo uliopangwa katika mpangilio maalumukwenda juu katika ghala lakuhifadhia mizigo, mfano mchele, mahindi, unga na bidhaa nyingine. | Ni tamko la mvuvi wakati mshipi wake umiliwa na samaki akiwa anavua.  |
| Hobesi         | Lugha ya kuhimiza kazi ya kutoa mzigo melini kwenda juu ya gati kwa kuunyanyua.   | Ni sauti ya kawaida isiyo na maana rasmi.   |
| Tani           | Ni kipimo maalumu cha uzito wa mizigo kutoka melini au ndani ya jahazi.   | Ni kipimo cha uzito.  |
| Mtilie mwezako | Amri ya kumsaidia mchukuzi mwezakoinayotolewa na chepe wa machukuzi.  | Ni kitendo cha kumtaka/ kumuomba mtu wa pili kuchukua kitu fulani na kukiingiza katika chombo au kifaa kingine kwa lengo la kukihifadhi katika hali ya kumsaidia. |
| Kam-pigaaa     | Kasaidiwa kukamilisha kazi ya ubebaji wa mizigo.  | Ni kitendo cha kutumia bakora au kifaa kingine na kumpiga mtu mwingine.   |
| Watehmani      | Mlinzi anayelinda makuli bandarini.   | Neno lenye maana nyingi,  |

**Kiambatanisho3: Mazungumzo na Makuli**

Mtafiti: Baba hili sumari lenye kupinda nchani lina mpini wa kunia linaitwaje, na kazi yake.

Kuli: Mwanangu hilo linaitwa “HOKO” na kazi yake ni kuzuia mzigo wakati wa kuweka begani na pia kuukamatia usianguke hadi unakokwenda,

Mtafiti: Haya baba ukiwa na mzigo na mbele huoni vizuri kama Yule anayekuja mbele ameinama kwa gunia unawapa,

Kuli: Mwanangu hapa ukiwa na mzigo wewe sema tu “nipe nyuma “au vumba vipi habari waliombe yako ili usiwaingilie hilo vumba hilo watakupa njia tu.

Mtafiti: Baba Yale magunia huwa mnapeleka wapi na huko muna yaweka vipi.

Kuli: Mwanangu nyie wasomi si kazi yenu huko kuna rasa, Rasa ya kwanza ya pili na nyengine, mwanangu hii ni kazi ya nguvu sana, \tunaofanya kama sisi tuliokosa ilimu n.k

**Kiambatanisho 4: Picha ya Bandari ya Unguja**

Muonekano wa mazingira tofauti ya bandari ya unguja ambapo makuli hufanya kazi ya uchukuzi wa mizigo, Hiki ni aina ya kifaa kinachoitwa rikwama ambacho kuli hutumia katika kubebea mzigo ulio mzito zaidi ya uwezo wake na pia unaosafiri masafa marefu huku akitumia rejista tofauti mfano samile huko, nipe nyuma , kaakand , vumba hilo na mengineyo.



**Chanzo: Mtafiti (2018)**



**Chanzo: Mtafiti (2018)**

**Makuli wakiwa bandarini wakikokota na kubeba mizigo kwa kutumia rikwama na mabega yao na kuusafirisha mzigo huo hadi kwa tajiri mwenye mzigo huo.**












**Makuli wakiwa pamoja na abiria wakishuka kutoka botini wakitokea Dar – salaam huku wakitekeleza wajibu wao wa kubeba mizigo ya abiria wakiwasiliana kwa kutumia rejista yao ile ile ya bandarini.**





Boti ya abiria ikiwasili bandarini Zanzibar makuli wakiwa tayari kupakuwa mizigo huku wakitumia rejiata yao. Maneno kama kaa kando, vumba hilo. Sumile hapo n.k

